# Nipashe

Jumanne Oktoba 27, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580381

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba :+255716500500
Barua Pepe:circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020


**WANAFA-MILIA** 3 wafia bwawani

UKURASA 7



**JPM** akabidhi msikiti, Lissu afanya maombi

UKURASA 2,3




# Wazanzibari kuanza maamuzi magumu leo

• **Jeshi** la Polisi latoa onyo kali kwa watakaofanya vurugu... *Endelea uk.17*


Bernard Membe-ACT


Twalib Ibrahim-UPDP


Seif Maalim- AAFP


John Shibuda-ADA-TADEA


Queen Sendiga-ADC


John Magufuli-CCM


Tundu Lissu-CHADEMA

## Mwenyekiti CHADEMA adaiwa kutekwa, kung'olewa meno

UKURASA 3


Yeremia Maganja-NCCR-Mageuzi


Leopold Mahona -NRA


Hashim Rungwe -CHAUMA


Ibrahim Lipumba-CUF


Philipo John Fumbo-DP




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Mchuano dakika za mwisho

UK. 2


Khalfani Mohamed Mazarui-UMD


Cecilia Mwanga-Demokrasia Makini


Mutamwega Migahwya-SAU


MICHEZO SIMBA YAPAPASWA, AZAM IKIFIA MTIBWA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# JPM asisitiza amani, umoja, mshikamano

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

RAIS John Magufuli amewataka Watanzania kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano kwa kuwa ndiyo nguzo pekee ya maendeleo iliyoasisiwa na hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Amesema Tanzania ndiyo taifa pekee ambalo watu wake hawajitambulishi kwa udini, ukabila wala ukanda, bali wanajitambulisha kwa utanzania.

Aliyasema hayo jana wilayani Chamwino, jijini Dodoma, wakati akizindua msikiti wa Sheikh Aboubakar Zuber bin Ali, ambao ulijengwa baada ya kuendesha harambee Agosti 23, mwaka huu, akiwa katika Kanisa la Katoliki Maria Emmaculate, kupatikana Sh. milioni 319.280.

"Kuna nchi zimeingia katika vita kwa sababu ya udini, ukabila, rangi, lakini sisi Tanzania Mungu ametujalia kuishi wa umoja na mshikamano bila ya kubaguana. Leo katika familia zetu kuna Waislamu, Wakristo, Wachaga, kuna familia mama Mkristo mtoto Mwislamu," alisema Rais Magufuli.

Alisema sifa hiyo haikuja kwa bahati mbaya bali ililetwa na viongozi waasisi wa taifa na wengine ambao wametangulia mbele ya haki.

"Agosti 23, niliendesha harambee ya ujenzi wa msikiti huu nikiwa kanisani, waumini waliokuwapo walichangia na kupatikana zaidi ya Sh. milioni 319, hii ni uthibitisho kuwa nchi hii haina ubaguzi wa dini."

Rais Magufuli alisema kukamilika kwa msikiti huo ukawajenge Watanzania na kuwa ndugu, wakakae pamoja, ukawaweke wananchi wa Chamwino pamoja, ukatoe mafunzo ambayo yatajenga umoja kwa Watanzania.

Pia, alisema kwa msitiki huo kukawe ni alama kwa Tanzania kwamba kulikuwapo na Sheikh ambaye aliwajenga Watanzania kwa umoja.

"Fedha iliyobakia katika ujenzi wa msikiti huu ikaanzishe harambee nyingine ya ujenzi wa kanisa wanaosali Jumamosi, nitafurahi siku moja nikiona Ikulu hii ikizungukwa na makanisa, misikiti," alisema Rais Magufuli.

Naye Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali, Charles Mbuge, alisema ujenzi wa msikiti huo ulianza Agosti 28, mwaka huu, na umegharimu Sh. milioni 319.280 na kwamba Sh. milioni 1.193 zimebaki katika akaunti.

Alisema msikiti huo utakaokuwa na uwezo wa kuchukua waumini zaidi ya 500, umejengwa kwa muda wa mwezi mmoja na siku 28 na wa awali ulikuwa na uwezo wa kuchukua waumini 150.

Kwa upande wake, Mufti Mkuu, Sheikh Aboubakar Zuber bin Ali, alisema: "Tunawashukuru Watanzania wote waliomuunga mkono Rais Magufuli katika ujenzi wa msikiti huu, pia tunampongeza kwa kurudisha mali za Waislamu zilizopotea, ujenzi wa msikiti mkubwa wa kimataifa eneo la Kinondoni Dar es Salaam."

■**Imeandaliwa na Gwamaka Alipipi na Augusta Njoji**



Rais Dk. John Magufuli akishirikiana pamoja na Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir Bin Ally (aliyekuwa mgeni rasmi), kufungua kitambaa kwenye jiwe la msingi, wakati wa ufunguzi rasmi wa msikiti wa Chamwino, uliofanyika jana, jijini Dodoma. **PICHA: IKULU**

# Mchuano wagombea dakika za mwisho

**Na Mwandishi Wetu**

KESHO Watanzania kote nchini watafanya uamuzi katika sanduku la kura kumchagua kiongozi wanayemtaka kuwaongoza kwa upande wa mgombea urais, ubunge na udiwani kwa miaka mitano ijayo.

Uamuzi huo unakuja baada ya siku 64 za kampeni za wagombea kujinadi kwa sera na ilani za vyama vyao na wananchi kuwasikiliza ili kuamua kutokana na ahadi zilizotolewa.

Kwa upande wa Tanzania Bara, wagombea leo wanatupa karata yao ya mwisho wakati wakihitimisha kampeni zao rasmi na upande wa Tanzania Visiwani, wanaanza kupiga kura ya mapema.

Wagombea wengi wamefanya kampeni zao kulingana na ratiba iliyotolewa na Tume ya Taifa Uchaguzi (NEC), huku wengine wakituma wasaidizi wao kuwawakilisha kwenye mikoa ambayo hawakuweza kufika.

Licha ya kilio cha ukata wa fedha kwa baadhi ya vyama, matukio kadhaa ya ukiukwaji wa mwongozo wa kampeni yameripotiwa katika maeneo mbalimbali.

Baadhi ya maeneo kumeripotiwa wanachama wa vyama kushambuliwa, kushambuliana, kufanya uharibifu wa mali na wengine kuuawa.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC, leo (Oktoba 27), wagombea watano wa vyama vya upinzani watahitimisha kampeni zao jijini Dar es Salaam, akiwamo wa Chama cha ADC ambaye atafanya mikutano wilaya za Ilala na Kigamboni kwa kutembelea kata zote.

Mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu na mgombea mwenza, Salum Mwalimu, atahitimisha kampeni zake katika Wilaya ya Kinondoni, na katika mikutano yake amesikika kuwa utakuwa katika Jimbo la Kawe.

Chama cha Wananchi (CUF), ambacho mgombea wake ni Prof. Ibrahim Lipumba, kitahitimisha kampeni zake katika viwanja vya Mwembe Yanga, Jimbo la Temeke.

Chama cha CHAUMMA, mgombea urais na makamu wake watafungia kampeni zao mkoa ya Dar es Salaam kata za Ubungo na Pwani kata za Rufiji na Mkuranga.

Kwa upande wa mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, atafungia kampeni zake jijini Dodoma maeneo ya Chamwino, huku mgombea mwenza akifungia kampeni mkoani Morogoro katika kata zote.

Mgombea wa Chama cha UMD atafungia kampeni zake katika Jimbo la Temeke, viwanja vya Zakhiem, jijini Dar es Salaam.

Ratiba hiyo ya NEC ilionyesha kuwa mgombea urais wa AAFP atafungia kampeni zake mkoani Songwe Kata ya Momba, huku ACT - Wazalendo kikifunga mkoani Lindi Kata ya Nachingwea.

Kwa upande wa mgombea wa ADA-TADEA, atahitimisha mkoani Simiyu, Kata ya Maswa, huku mgombea urais wa Demokrasia Makini akifunga kampeni zake mkoani Iringa.

Mgombea urais wa DP na mgombea mwenza watahitimisha mkoani Songwe, Wilaya ya Mbozi, huku mgombea urais wa NCCR-Mageuzi akifunga mkoani Mara katika Wilaya ya Bunda.

Pia, mgombea mwenza wa NCCR - Mageuzi atakuwa mkoani Pwani, Wilaya ya Kibaha, kuhitimisha.

Chama cha SAU kitafunga kampeni zake mkoani Mara, huku mgombea urais wa UPDP atakuwa mkoani Mbeya.

Kwa upande wa mgombea urais wa NRA, atakuwa mkoani Kigoma na mgombea mwenza mkoani Tanga.

**CCM NA MAJIMBO**

Kwa mujibu wa NEC wagombea ubunge wa CCM katika majimbo 28 wamepita bila kupingwa na madiwani wa kata 870 pia wamepita bila kupingwa.

## Wafuasi CCM, CHADEMA wadaiwa kushambuliana Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

GARI la matangazo la mgombea ubunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini kupitia CCM, Patrobas Katambi, linadaiwa kushambuliwa kwa kupigwa mawe na kuvunjwa vioo vyote.

Pia yamo magari mawili ya makada wa CCM, kwenye vurugu kati ya wafuasi wa CCM na CHADEMA, huku baadhi ya watu wakidaiwa kujeruhiwa.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alitoa taarifa hiyo juzi kwa vyombo vya habari, kuwa tukio hilo limetokea Oktoba 25, mwaka huu, majira ya saa moja jioni, baada ya wafuasi wa CHADEMA na CCM, kukutana eneo moja wakiwa katika maandamano ndipo vurugu zikaanza.

Alisema vurugu hizo zilisababisha uharibifu wa mali, na baadhi ya watu kujeruhiwa, ambapo mbali na gari la matangazo la Katambi, kushambuliwa, pia gari la Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Dotto Joshua, lilivunjwa kioo cha mbele pamoja na gari la Cecilia Sangaluka lililovunjwa indicator.

"Wafuasi hawa wa CHADEMA na CCM walikutana eneo la Japanise Corner wakiwa na wagombea wao wa ubunge, wakiwasindikiza kwa maandamano kutoka kwenye maeneo yao ya kampeni hadi ofisi za vyama vyao, ndipo vurugu zikaanza na kusababisha uharibifu wa mali na watu kujeruhiwa," alisema Magiligimba.

Aidha, alisema jeshi hilo linawashikilia watu watano kwa tuhuma za kuhusika na vurugu hizo, ambao ni Ramadhani Mohamed, Yuda Kanoku, Frank Chiza, Timoth Amosi, na Mussa Luhende.

Alisema baada ya upelelezi kukamilika, watafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Katika hatua nyingine, Kamanda Magiligimba aliwahakikishia wananchi wa mkoa huo kuwa amani itakuwapo kesho siku ya kupiga kura, na kwamba jeshi limejipanga vyema kudhibiti watu watakaotishia amani.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Mayanga Contractors, Mhandisi Stephen Makigo, akitoa mada kuhusu namna makandarasi wanavyoweza kuungana kutekeleza miradi mbalimbali kwenye mafunzo ya siku moja yaliyoandaliwa na Bodi ya Makandarasi Nchini (CRB), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Lissu, CHADEMA wafanya maombi maalum

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akiwamo mgombea wake wa urais wa Jamhuri ya Muungano, Tundu Lissu, jana kilijikita katika maombi maalum ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika kesho.

Pamoja na mambo mengine, lengo ni kuwaombea mgombea urais na mgombea mwenza kuelekea uchaguzi mkuu.

Aidha, chama hicho pia kimefanya maombi kwa ajili ya wagombea wa nafasi za ubunge, udiwani pamoja na mamlaka za usimamizi wa uchaguzi na vyombo vya dola ili kuwapo na haki katika uchaguzi huo.

Katika ukurasa wake wa twitter, Lissu aliandika kwamba: "Kuelekea siku ya uchaguzi 2020, natoa wito kwa Watanzania wote, wa dini zote na madhehebu yote tuungane kwenye sala, dua maombi ili tuwe na uchaguzi huru na haki kwa manufaa ya taifa letu," alisema Lissu.

Kwa mujibu wa CHADEMA, mambo mengine waliyoombea ni mawakala ili watimize wajibu wao, ikiwamo kutokubali kuhujumiwa.

Baadhi ya viongozi wa dini walinakiliwa kushiriki katika maombi hayo na picha zao kutumika. Maombi hayo yalianzia Mang`onyi mkoani Singida ambako Lissu alianzia kwa kuzungumza na wananchi akielekea katika mikutano yake ya kampeni katika kumalizia ng`we ya lala salama.

Katika mkutano huo Lissu aliomba wafuasi wa chama chake kuhakikisha wanawahudumia mawakala katika vituo vyote vya kupigia kura.

"Ninawaomba mhakikishe mnawahudumia mawakala wetu, wakihitaji maji, chakula muwapelekee, msiwaache wapate shida," alisema.

# Cheyo amnadi Magufuli kanisani

**Na Happy Severine,** BARIADI

MWENYEKITI wa Chama cha United Democratic Party (UDP), John Cheyo, amesema yeye na chama chake wataendelea kumwombea kura Rais John Magufuli katika uchaguzi mkuu utakaofanyika kesho.

Cheyo alisema hayo Jumapili wakati wa ibada ya misa takatifu iliyofanyika katika Kanisa la Katoliki la Mt. Luka mjini Bariadi.

Alisema rais si chama na yeye hachagui chama bali anachagua mtu, na kwamba Rais Magufuli ana uwezo wa kuongoza nchi na ndiyo maana ameamua kuja Bariadi kwa lengo la kumpigia kampeni ili ashinde, huku akiwaomba wananchi wampigie kura ashinde.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Taifa, Kheri James, alisema CCM haitakubali kutoa uhuru kwa ndoa za jinsia moja hata kama wananchi hao watakataa kukichagua chama hicho.

Alisema hayo mkoani Simiyu, wakati wa kampeni ya mgombea ubunge wa Jimbo la Bariadi, Andrea Kundo, zilizofanyika katika Kijiji cha Igaganulwa katika Kata ya Dutwa.

Alisema serikali ya awamu ya tano ambayo imeleta na kujenga uhuru, amani na maendeleo kwa wananchi wake, haitaruhusu ushoga kwani Tanzania haina tamaduni hizo na hairuhusu mambo hayo kufanyika.

Aidha, aliwataka wananchi wa Bariadi kumchagua Kundo kuwa mbunge ili aweze kuendeleza kazi zilizoachwa na mtangulizi wake, Andrew Chenge.

Kwa upande wake, Kundo alisema kuwa endapo atachaguliwa kuwa mbunge, atapenda kupimwa kwa mambo yatakayokuwa na Rais Magufuli, lakini pia apimwe kwa kile atakachoahidi na kukitekeleza kwa maendeleo ya Watanzania.

# Mwenyekiti CHADEMA adaiwa kutekwa, kung'olewa meno

**Na Thobias Mwanakatwe,** KYELA

IKIWA imebakia siku moja kabla uchaguzi mkuu kufanyika, vurugu za kisiasa zimejitokeza Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, baada ya Mwenyekiti wa CHADEMA Kata ya Matema kudaiwa kutekwa kujeruhiwa na kuvunjwa meno mawili na watu watano ambao wametiwa mbaroni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akizungumza na gazeti hili alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba watuhumiwa watano wanaoshukiwa kuhusika wamekamatwa. "Tumewakamata watuhumiwa watano, na hivi sasa mwanasheria wa sheria anashughulikia hilo ili watuhumiwa waweze kufikishwa mahakamani," alisema Matei.

Mwenyekiti huyo Kened Matomola (50), akizungumza na gazeti hili jana katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela ambako amelazwa, alisema alitekwa na watu zaidi ya 8 Oktoba 23, mwaka huu saa 10:30 katika kitongoji cha Lyulilo Kijiji cha Ikombe, Kata ya Matema.

Matomola alisema siku ya tukio alikuwa katika kijiji cha Ikombe kwa ajili ya kufanya maandalizi ya mkutano wa kampeni za mgombea ubunge Jimbo la Kyela, Ali-nanuswe Mwalwage, ambao ulikuwa ufanyike Oktoba 24.

Alisema akiwa katika kijiji hicho, ghafla ilifika gari aina ya Noah yenye rangi nyeusi ikiwa na maandishi yaliyosomeka 'Mama ni Mjomba' ambayo waliteremka watu 8 na kumzunguka kisha kumkamata.

Matomola alisema watu hao baada ya kumkamata walimwingiza kwa nguvu katika gari hilo na likaondoka ambapo alijaribu kupiga kelele kuomba msaada bila mafanikio. Alisema akiwa chini ya ulinzi ndani ya gari hilo watekaji walimfunga mkono na mguu wa kushoto kwa kamba na kumweka kwenye buti ya gari kisha kuanza kumpiga kwa nondo na virungu ambapo walimvunja meno mawili na kumtengua kiuno.

Matomola alisema watu ambao hawafahamu, wakati wanampiga walikuwa wakimwambia kuwa anawasumbua sana katika uchaguzi huu na kwamba sasa mwisho wake umefika.

Aliongeza kuwa gari lililombeba lilifika katika ofisi za chama kimoja, lakini baadaye viongozi wa CHADEMA walipata taarifa za kutekwa kwake ambapo walikwenda kutoa taarifa polisi.

Alisema polisi walifika katika ofisi za chama hicho na kuwakamata watuhumiwa watano saa 2:00 usiku.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P 2888,**
**40470 DODOMA**
**Tarehe 26/10/2020**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMANNE** tarehe 27-10-2020 kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 175 DFN / T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.00 |
| Upana | - | mita | 3.00 |
| Kimo | - | mita | 5.00 |

3. Njia itakayotumika: **SINGIDA** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MOROGORO.**

   Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Majaliwa awaasa wananchi wasichague kwa hasira

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania wasichague kiongozi kwa sababu ya jazba au hasira.

Alitoa wito huo jana, wakati akizungumza na wakazi wa kata ya Nalasi, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma katika mkutano uliofanyika kwenye viwanja vya Katani. Majaliwa jana alizuru Wilaya ya Tunduru akimwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli.

"Hatuendi kwenye chama kwa jazba wala kwa hasira. Hatari ya kipindi hiki unaweza kujikuta unaenda kwenye chama ambacho hakina sera wala hakieleweki. Chama makini kinapaswa kuwa na viongozi wanaoeleweka," alisema.

Akitoa mfano, Majaliwa alisema jana kuna chama viongozi wake wamegombana na wala hakina mgombea urais. "Je, ukikichagua chama hiki na ukawa na changamoto inakukabili, utaipeleka wapi? Au utampelekea nani? Na ukimchagua diwani au mbunge wa chama hicho, hayo masuala yako atayawakilisha kwa nani?"

"Ninawasihi, unapochagua viongozi, usichague chama kwa sababu maendeleo hayana chama. Chagueni chama ambacho kina mwelekeo na kinajali kutatua shida za watu. Ukienda kupiga kura, chagua diwani, mbunge na rais anayetoka Chama Cha Mapinduzi. Keshokutwa (kesho), tumchague Dk. Magufuli kwa kura nyingi za ndiyo," alisisitiza.

Majaliwa pia, aliwaombea kura mgombea ubunge wa Jimbo la Tunduru Kusini, Adimu Mpakate na wagombea udiwani wa kata nne za jimbo hilo.

Akiwa njiani kuelekea Tunduru, alifanya mkutano wa hadhara katika viwanja vya stendi ya mabasi ya Mangaka, wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara, aliwasihi Watanzania wasikubali kuandamana kwa kisingizio cha kutokubali matokeo ya uchaguzi kwa sababu huko ni kuvunja sheria.

"Ninawasihi vijana mjihadhari, msikubali kuandamana kwa kuwa mtakuwa mnavunja sheria na mtajikuta mnajiingiza matatizoni. Kuna mtu anakuja hapa na anatulazimisha kuandamana, huyo hafai kuwa rais wa nchi."




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe (katikati), akipokea kitabu kijulikanacho kwa jina la Kwa Nini Aman? kutoka kwa Rais wa Taasisi ya Al-Hikma Foundation, Abdulqadir Al-Ahdal (kushoto), kilichoandikwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Sheikh. Nurdeen Kishk (kulia), katika hafla ya dua maalum ilioombwa na waumini wa dini ya kiislam katika kuliombea taifa amani iliyoandaliwa na taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtendaji jela mwaka 1 kwa kutoa ushahidi wa uongo

**Na Joctan Ngelly**, GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita, imemhukumu Mtendaji wa Kijiji cha Mabila, Ferdinand Tanganyika (50), kifungo cha miezi 12 au kulipa faini ya Sh. 300,000 kwa kosa la kutoa ushahidi wa uongo mahakamani.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo. Hakimu Kiiza alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na viongozi wengine wenye tabia ya kusema uongo kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Geita, Hasna Kiboko, ulipeleka mahakamani mashahidi wanne na vielelezo saba ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitoa ushahidi wa uongo.

Alisema Juni 14, 2019 katika mahakama hiyo, mshtakiwa huyo akiwa shahidi wa upande wa mashtaka wa TAKUKURU, katika shauri la jinai lililomhusu Salumu Mhanga, Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Kata ya Makurugusi, aliyekuwa ameshtakiwa kwa makosa ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 100,000, mshtakiwa akiwa shahidi muhimu wa upande wa Jamhuri alitoa ushahidi wa uongo akijua kuwa anayoyasema ni ya uongo.

Alisema, upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa TAKUKURU, Hasna Kiboko, walimfungulia kesi mshtakiwa Tanganyika kwa kutoa ushahidi wa uongo mahakamani.

Alisema katika kesi hiyo upande wa mshtaka ulipeleka mashahidi wanne na vilelezo vinne ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitoa ushahidi wa uongo.

Akijitetea baada ya kuhumu hiyo, mshtakiwa huyo alidai: "Mimi nina familia ya watu nane, vile vile, mwaka jana kaka yangu alifariki dunia na kuniachia watoto tisa, mimi ninaishi na virusi vya ukimwi naomba mahakama hii inipunguzie adhabu."

Hakimu Kiiza alitupilia mbali utetezi huo na kusema mshtakiwa akiwa mtumishi wa umma amekiuka kiapo na atatumikia kifungo cha miezi 12 jela au kulipa faini ya Sh. 300,000.

Mshtakiwa huyo aliachiwa huru na mahakama hiyo baada ya kulipa faini.

# Mdee ajinadi alivyotatua mgogoro sugu wa ardhi

**Na Enock Charles**

MGOMBEA ubunge kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika Jimbo la Kawe, Halima Mdee, amejigamba kuwa katika miaka takriban 10 ya ubunge wake katika jimbo hilo, alifanikiwa kutatua migogoro ya ardhi aliyoiita kuwa ni sugu.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Mdee ameeleza kuwa wakati anapata ubunge katika jimbo hilo kwa mara ya kwanza, alikutana na migogoro ya ardhi ya muda mrefu, na kwamba ilikuwa ni tatizo kubwa kwa baadhi ya wananchi jimboni hapo, jambo lilosababisha wananchi hao kumfuata mara kadhaa ofisini kwake kusaka ufumbuzi.

"Hili jimbo lilikuwa chini ya Chama Cha Mapinduzi kwa miaka 50 wakati sisi tunachukua dhamana miaka 10 iliyopita, suala la migogoro ya ardhi iliyokuwa sugu chini ya utawala wa CCM, tumeweza kuitatua yote kwa miaka 10 ya uongozi wa CHADEMA lilikuwa ni tatizo kubwa," alisema Mdee.

Licha ya migogoro ya ardhi, pia alisema barabara katika jimbo hilo hasa zile za kuunganisha kata moja na nyingine zilikuwa hazipitiki kirahisi, na kujigamba kuwa katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake kupitia CHADEMA ameweza kurekebisha barabara hizo, huku zingine ujenzi ukiendelea.

"Barabara zilikuwa korofi katika kata karibia zote, barabara muhimu za kuunganisha kata zetu na mji tumezirekebisha, na ujenzi unaendelea...kulikuwa kuna shida ya maji karibia robo tatu ya kata tofauti na hali ilivyo sasa," aliongeza Mdee.

## TANGAZO

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFAZA FEDHA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,677 | 1,693 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,049 | 20,731 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 51,020 | 46,085 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,671 | 2,371 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 20,411 | 7,349 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 72,450 | 71,319 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,067 | 4,101 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,350 | 677 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **166,695** | **154,326** |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 57,151 | 44,151 |
| 18 | Amana za Wateja | 68,810 | 70,057 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 29 | 47 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 25 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,363 | 2,331 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,046 | 2,081 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **130,424** | **118,692** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **36,271** | **35,634** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,328 | 3,457 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 10,201 | 10,072 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,242 | 605 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **36,271** | **35,634** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 3,280 | 5,248 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,307 | 6,307 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,858 | 2,611 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 21.76% | 23.09% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.38% | 8.53% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 59.79% | 64.73% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 43.46% | 46.21% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.03% | 82.53% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 10.29% | 1.39% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 8.01% | 0.75% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 3,089 | 3,240 | 9,299 | 9,200 |
| 2 Gharama za Riba | 1,225 | 1,240 | 3,719 | 3,663 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,864** | **2,000** | **5,580** | **5,537** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | 7 | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 252 | 233 | 931 | 161 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **210** | **332** | **510** | **789** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 44 | 51 | 154 | 188 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 166 | 281 | 356 | 601 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,186** | **1,304** | **3,373** | **3,213** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 426 | 403 | 1,287 | 1,222 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 760 | 901 | 2,086 | 1,991 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **636** | **795** | **1,779** | **2,952** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | - | 240 | 537 | 720 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **636** | **555** | **1,242** | **2,232** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya** | **636** | **555** | **1,242** | **2,232** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 30 | 28 | 30 | 28 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 118 | 103 | 77 | 138 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.59% | 2.91% | 1.53% | 2.67% |
| (ii) Wanahisa | 7.05% | 6.25% | 4.62% | 8.51% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 35.95% | 36.51% | 34.39% | 32.17% |
| (iv) Zinazozalisha | 5.52% | 6.23% | 5.64% | 5.90% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.07.2020** | 21,500 | - | 10,677 | 3,457 | - | - | **35,635** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 636 | - | - | - | **636** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 129 | (129) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | - | | | | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.09.2020** | **21,500** | **-** | **11,442** | **3,328** | **-** | **-** | **36,271** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.04.2020** | **21,500** | **-** | **10,576** | **3,575** | **-** | **-** | **35,651** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 331 | - | - | - | 331 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 118 | (118) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (348) | - | - | - | **(348)** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.06.2020** | **21,500** | **-** | **10,677** | **3,457** | **-** | **-** | **35,634** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 636 | 600 | 1,779 | 2,952 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 439 | 444 | 1,110 | 307 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,364) | 986 | (4,123) | (4,546) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 11,753 | 1,562 | 18,803 | (11,379) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (3,917) | (3,114) | (5,873) | 2,813 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (21) | (403) | (1,111) | 530 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2,161) | (3,201) | (2,243) | 483 |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | (617) | (537) | (720) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za*** | ***5,365*** | ***(3,743)*** | ***7,805*** | ***(9,560)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (132) | (0) | (149) | (100) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(132)*** | ***(0)*** | ***(149)*** | ***(100)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - | - | - |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **5,233** | **(3,743)** | **7,657** | **(9,660)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 25,856 | 29,599 | 23,432 | 34,685 |
| | **Robo Mwaka** | **31,089** | **25,856** | **31,089** | **25,025** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020**

**Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Ashwani Kumar Negi<br>Mkurugenzi Mkuu | | 20.10.2020 |
| Mr. Heriabdiel Ayoh<br>Mkuu wa Fedha | | 20.10.2020 |
| Mr. Allen Richard<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | | 20.10.2020 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Dr. Bernard E. Mnzava - Director | | 20.10.2020 |
| 2. Mr. Suitbert Kageuka - Director | | 20.10.2020 |

## DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | Up to Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | Over 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | Up to 5000 USD a day | free | - |
| | Over 5000 USD withdrawal | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | Deposit fee | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | **Current account.** | | |
| | (Up to USD 10000) | Free | - |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| a) | Saving bank customer ID Card-one time | 7 | 10,000 |
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| **3.0** | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| **4.0** | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| | | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | - Individual | USD 3.00 (USD a/c)<br>TZS 5,000 (TZS a/c) | 1st 50 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS<br>TZS 100 per SMS |
| | - Corporate | USD 10.00 (USD a/c)<br>TZS 15,000 (TZS a/c) | 1st 150 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS<br>TZS 100 per SMS |

| | | | |
|---|---|---|---|
| e) | Others | - | - |
| **5.0** | **Foreign Exchange Transaction.** | - | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | |
| | | A/C holder / Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 / 40 | -- |
| | USD 6001-10,000 | 30 | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | |
| **6.0** | **Other Charges** | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | |
| | - Individuals | 3 | 5,000 |
| | - Corporate | 6 | 12,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **7.0** | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| **8.0** | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| **9.0** | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| **10.0** | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |

No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the period covered by the disclosure

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 20.10. 2020 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | Head of Finance | Signed | 20.10. 2020 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 20.10. 2020 |

### OTHER DISCLOSURES (VIAMBATANISHI

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 14.00% p.a. |
| **2.0** | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 4.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| **5.0** | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 6.50% |
| | Over 6 months | 2.50% | 7.50% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 7.00% |
| | Over 6 months | 3.00% | 8.00% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 20.10. 2020 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | Head of Finance | Signed | 20.10. 2020 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 20.10. 2020 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kura ya mapema Zanzibar, kila mmoja atimize wajibu wake

**WANANCHI** wa Visiwa vya Zanzibar leo wanaanza kufanya maamuzi ndani ya sanduku la kura kwa kupiga kura kwa mujibu wa utaratibu kwa watu maalum ambao wanakuwa na majukumu mengi siku ya kesho.

Kura hiyo inajulikana kama kura ya mapema ikiwa ni hatua ya mwanzo ya kufanya maamuzi ndani ya sanduku la kura juu ya nani anafaa kuongoza kwa nafasi ya shehia, uwakilishi na urais wa visiwa hivyo.

Aidha, Jeshi la Polisi limewaonya wananchi ambao kwa namna moja au nyingine watajihusisha na vitendo vya uvunjifu wa amani, na kwamba hatua zaidi zitachukuliwa dhidi yao.

Baadhi ya wanasiasa wamewahamasisha wananchi kwenda kwenye vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kupiga kura, lakini Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na vyombo vya dola vimewaonya na kuwataka kuwa makini na kuzingatia sheria.

Kipindi cha uchaguzi ndicho ambacho taifa hugawanyika vipande ikiwa nafasi hiyo itatolewa na washiriki wote wa uchaguzi kwa maana ya wachezaji, refa na washangaliaji.

Tangu awali vyama vya upinzani vilipaza sauti kupinga kura ya mapema inayohusisha makundi maalum, huku wakieleza wasiwasi wao juu ya utekelezaji wake na wakitaka baadhi ya wananchi wahusishwe.

Aidha, mamia ya wananchi walijitokeza kulalamika kutoandikishwa katika daftari ya mpigakura kutokana na kukosa vitambulisho vya Mzanzibar mkaazi, jambo ambalo linawanyima haki yao ya kupiga kura.

Mara kadhaa ZEC imetoa ufafanuzi kura hiyo ni kwa makundi ambayo siku ya uchaguzi mkuu atakuwa na majukumu ya kusimamia na kulinda amani.

Kasoro mbalimbali zimeibuliwa katika daftari la kudumu la wapigakura Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na ZEC wametoa ufafanuzi, ambao wadau wa uchaguzi wa vyama vya upinzani wameonyesha kutokubaliana nao.

Sisi tunazishauri mamlaka zote kuhakikisha zinatenda haki na kuwa chachu ya amani kwa kuwa malalamiko mengi yanaelekezwa kwao kwa kila upande kuona hautendewi haki.

Ni wajibu wa kila Mzanzibari kuhakikisha uchaguzi unamalizika salama na pasiwe na kuvunjika kwa amani au watu kujeruhiwa na kupoteza maisha.

Zipo nchi zilizojikuta katika wakati mgumu kwa muda mrefu na baadhi zilifanikiwa kusuluhisha na kurudi kwenye amani, lakini zipo ambazo misingi ya amani ilitikisika na maadui walipata mwanya wa kuwavuruga zaidi na hawakuwahi kurudi kwenye mstari.

Utekelezaji wa kura ya maoni utatoa picha halisi ya uchaguzi kwa ujumla visiwani humo, na hatua za kuchukua, lakini bado malalamiko ya msingi lazima yafanyiwe kazi.

Vyama vya siasa vina wajibu wa kuhakikisha amani muda wote kwa kuwatuliza wafuasi wao, ili taifa lisitumbukie katika machafuko ambayo yataigharimu nchi.

Viongozi wa dini nao wana wajibu mkubwa kulisaidia taifa, kwa maombi na kuwatuliza wafuasi wa vyama ikiwa haki itakuwa imesimamia na kutendeka.

Uchaguzu usigawe visiwa hivyo, bali uliunganishe taifa kwa kuwa uongozi wa watu utakuwa na maana zaidi ikiwa tu hauongozi watu ambao wamepoteza mamia ya wapendwa wao au kujeruhiwa.

Kwa vyombo vya ulinzi vinapaswa kuwa huru pasipo kupendelea upande wowote bali kutenda haki kwa wote kwa kuwa wananchi ndiyo waamuzi kupitia sanduku la kura juu ya nani awe kiongozi wao katika eneo au taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mfululizo moto kuteketeza mabweni, kuua ukomeshwe

Na Sabato Kasika

**SIKU** za hivi karibuni kumekuwapo na mfululizo wa taarifa za mabweni ya wanafunzi katika shule mbalimbali kuteketea kwa moto, hali ambayo inatishia usalama wao na hata kukwamisha maendeleo ya elimu.

Mfano mmojawapo ni tukio la hivi karibuni la bweni ya Shule ya Sekondari Uchira Islamic Kilimanjaro, kuteketea.

Aidha, kumeripotiwa matukio kama hayo kwenye shule mbalimbali ikiwamo ya Kinondoni Islamic ya Dar es Salaam.

Kwa hali hiyo, ipo haja ya kuchunguza kwa kina kiini cha matukio hayo na kuchukua hatua za kuyakomesha ili wanafunzi waweze kusoma bila hofu na wasiwasi wa usalama wa maisha yao.

Muungwana anaamini kwamba, matukio hayo yanaweza kusababisha wanafunzi wakimbie shule na kushindwa kuhudhuria kikamilifu masomo shuleni na hivyo kushuka kitaaluma.

Ikumbukwe kuwa kuwapo kwa mabweni shuleni ni moja ya hatua ya kuwapunguzia wanafunzi kutembelea umbali mrefu kufuata elimu ama kuwaepusha wanafunzi wa kike na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Lakini, cha kushangaza ni kuwapo kwa matukio hayo ya mabweni kuteketezwa na moto, hali ambayo inawalazimu walimu kila mara kuwa na kazi ya kujenga wanafunzi kisaikolojia kutokana na matukio hayo.

Ni vyema wanaochoma mabweni wakatambua kuwa wanaleta uchungu kutokana na vifo vya wanafunzi wanaouliwa kwa bila hatia, lakini kuiingizia serikali hasara ya mamilioni ya fedha kwa vitendo hivyo visivyokubalika mbele ya jamii ambayo vinapaswa kulaaniwa.

Watu wanachoma shule na kusababisha vifo, majeruhi na hasara ya mamilioni ya pesa wanafanya vitendo hivyo ni wa kusakwa kwa nguvu zote kisha wachukuliwe hatua za kisheria.

Kwa mfano Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, aliwahi kuwachapa viboko wanafunzi watano waliohusika katika tukio la kuchoma moto Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Oswe.

Wanafunzi hao walisababisha hasara ya zaidi ya Sh. milioni 26, ambazo huenda zingetumika kwa shughuli nyingine za maendeleo ya shule.

Ni muhimu wanafunzi wakazingatia masomo na kuacha tabia za kujiingiza katika vitendo viovu vinavyoweza kuharibu maisha yao kwani taifa linawategemea wawe wananchi bora na viongozi ama watendaji wa baadaye.

Kama kuna watu wanawashawishi wanafunzi kujiingiza katika vitendo, ni bora wakaacha kwa kuwa wanawaharibia maisha yao ya baadaye, na pia wanafunzi wenyewe wanatakiwa kujiongeza na kujiweka kando na matendo maovu.

Wanafunzi wanaojiingiza katika matendo hayo, watambue wanajiandaa kuwa watu hatari wa baadaye, lakini wale wanaozingatia masomo, ni viongozi na wataalamu wa baadaye wa fani mbalimbali.

Vilevile ni muhimu wanafunzi watambue kuwa elimu ina kaulimbiu mbalimbali ikiwamo ya 'elimu ni ufunguo wa maisha', kwa maana kwamba, ukitaka kuwa na maisha mazuri ni lazima uwe na elimu nzuri kichwani.

Kwa hiyo wanafunzi wanapokwenda shuleni ama kuishi shuleni, wajue elimu ina upana wake ambao hauna uhusiano na matendo maovu kama hayo ya kuchoma mabweni kama ambavyo imekuwa ikitokea.

Wanafunzi wanatakiwa kuunda vikundi vya kuwezesha kujiongezea maarifa katika elimu na siyo kuandaa mipango ya kufanya uhalifu na kusababisha madhara na hasara kwa miundombinu ya shule.

Pamoja na hayo, kuna haja kwa mamlaka husika kufanya uchunguzi wa kina kuhusu matukio ya mfululizo ya uchomaji wa mabweni katika shule mbalimbali na kuchukua hatua zinazostahili kwa wahusika.

Inasikitisha kuona serikali inahangaika kuboresha elimu kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa elimu bure ili kila mtoto wa Kitanzania aweze kusoma, halafu wanajitokeza baadhi ya watu wanavuruga.

Muungwana anashauri kwamba, kila mdau wa elimu atoe ushirikiano ili kuwapata watu wanaojihusisha na vitendo hivyo vinavyohatarisha maisha ya wanafunzi na pia kuharibu maendeleo yao ya kielimu.

Kulikoni kuwapo kwa taarifa mfululizo za mabweni kuteketea kwa moto katika shule mbalimbali? Nyuma yake kuna nini. Wanafunzi waachwe huru wasome bila kuvurugwa na matukio hayo yanayoangamiza maisha.

# Bwawa laua watatu wa familia moja

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAKAZI watatu wa familia moja wa Kijiji cha Kerende Kata ya Kemambo wilayani Tarime mkoani Mara, wamekufa maji kwa kutumbukia kwenye bwawa la maji.

Wanafamilia hao ni Buhumbi Chacha (10), ambaye ni mwanafunzi darasa la pili Shule ya Msingi Kerende, Musa Kubyo (27) na Chacha Machori (16).

Buhumbi ndiye aliyeanza kuzama akiwa anawapeleka ng'ombe kuwanywesha maji na ndugu zake hao wawili Musa na Chacha walizama ndani ya tope na kufa walipokuwa wanajaribu kumuokoa mdogo wao.

Katibu Tawala Wilaya ya Tarime, John Marwa alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 24 mchana katika Kijiji cha Kerende kata ya Kemambo.

Alisema mmoja wao alipanda juu ya ng'ombe na kucheza naye ambapo alirushwa ndani ya maji marefu na kushindwa kuogelea kujiokoa ndipo wenzake waliokuwa nao walianza kupiga kelele za kuomba msaada. Alisema ndugu zake Buhumbi wakiwemo wazazi wake na wananchi walijitokeza kujaribu kumuokoa mwanafunzi huyo bila mafanikio na ndipo ndugu zake wawili Musa Kubyo na Chacha Machori walipojitosa kuogelea.

Alisema jitihada zao hazikufanikiwa na badala yake walizama ndani ya tope hali iliyosababisha nao wafariki.

# Ufaransa, EAC waingia makubaliano ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC), imesaini makubaliano (MoU) na serikali ya Ufaransa ya kuanzisha mfumo wa ushirikiano kimkakati kwa kupata wataalamu na kudumisha ajenda mbalimbali.

Makubaliano hayo yalisainiwa makao mkuu ya EAC jijini Arusha baina ya Ubalozi wa Ufaransa, Frederick Clavier na Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Liberat Mfumukeko.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari, makubaliano hayo yamelenga maeneo makuu matano ambayo pande zote zinataka kuona matokeo ambayo ni nishati, mabadiliko ya tabia nchi na bioanuwai, viwanda, maendeleo ya sekta binafsi na uwekezaji, huduma na biashara, sekta ya fedha na kuwajengea uwezo katika miradi ya maendeleo.

Aidha, katika utekelezaji wa makubaliano hayo na kuwafikia wadau muhimu, serikali ya Ufaransa itawaleta pamoja wadau wakuu wa maeneo yote.

Akizungumza wakati wa kusaini makubaliano hayo, Balozi wa Ufaransa aliyeambatana na Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) wa Afrika Mashariki, Christian Yoka, walijadiliana kwa kina na EAC namna pande zote zitafanya kazi vizuri katika kuziinua sekta muhimu katika kuboresha na kuinua maisha ya watu.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Mfumukeko, aliishukuru Ufaransa kwa kukubali kushirikiana katika jitihada mbalimbali na kwamba wamepiga hatua kubwa katika kila nguzo zake ikiwamo kuwa na ushirikiano katika eneo la forodha na itifaki.

Alisema kabla ya COVID-19, bishara ya ndani iliongezeka huku baina ya nchi na nchi zikipungua na kuanzisha mkakati maalum wa kuondoa vikwazo katika maeneo 13 ikiwamo kuondoa visa na kupungua kwa ada ya vibali vya kazi.

Jingine ni matumizi ya kadi za vitambulisho vya kimataifa kama hati ya kufiria katika baadhi ya nchi wanachama, hati ya kusafiria ya pamoja inayotambuliwa kimataifa.

Balozi wa Ufaransa, Clavier, alipongeza mafanikio yaliyopo hasa katika ushuru wa forodha kwa kuwa na soko la pamoja, na kwamba serikali yake itaunda mfumo kamili wa ushirikiano huku akieleza kuwa nchi hiyo imeshatoza zaidi ya Euro bilioni 2.3 kwa EAC kati yake Euro milioni 476.6 kwa Tanzania.

Alisema msaada wa Ufaransa umelenga kuharakisha mabadiliko ya ulimwengu kwa kusaidia miradi ya maji, kilimo, maendeleo ya miji, elimu na afya katika nchi 115.

"Katika miaka 10 iliyopita kiasi cha fedha kinachotolewa na AFD kiliongezeka kutoka Euro milioni 31 hadi 172 kwa miradi ya sekta ya maji na usafi wa mazingira, nishati, afya na hasa mradi wa maji na usafi wa mazingira wa Ziwa Viktoria uliogharimu Euro milioni 76.5, kukuza huduma za afya Euro milioni 10, mradi wa ukarabati wa Gridi ya Taifa na Usambazaji wa umeme Euro Milioni 53," alibainisha.


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe Nipashe mwendo mdundo
Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)
PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store Google Play
KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz nipashe TheGuardiantz YouTube TheGuardiantz

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | **SAVINGS ACCOUNTS** | **RETAIL** | **CORPORATE** |
| 1 | **FREEDOM SAVINGS** | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | **GENERAL SAVINGS** | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | **EMPLOYEE SAVINGS** | | **N/A** |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | **SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS** | | **N/A** |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | **SAVINGS ACCOUNT SALARY** | | **N/A** |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | **SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY** | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 5 | |
| 7 | **U-CARE CHILDREN SAVINGS** | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | **CURRENT ACCOUNTS** | | |
| 1 | **INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT** | | **BUSINESS CURRENT ACCOUNT** |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenence fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | **DIPLOMAT ACCOUNTS** | | |
| | Required minimum opening balance | USD 200 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenence fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | **DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | **DEPOSIT ACCOUNTS** | | |
| 1 | **Call Accounts** | | **Call Accounts** |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | **Term Deposits** | | **Term Deposits** |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | **ELECTRONIC BANKING** | | |
| 1 | **E-Banking** | | **E-Banking** |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 + 1.5% | N/A |
| 2 | **Visa Debit Card** | | **N/A** |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | **Visa Perapid Cards** | | **N/A** |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| 4 | **ATM Withdrawals** | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | |
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | **LOANS** | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | **TEMPORARY OVERDAFT (TODs)** | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | **TRADE FINANCE** | | |
| 1 | **Guarantees** | | **Guarantees** |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | **Letters of Credit - Imports** | | **Letters of Credit - Imports** |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | **Letters of Credit - Exports** | | **Letters of Credit - Exports** |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | **Letters of Credit Refinancing** | | **Letters of Credit Refinancing** |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | **Discounting on LC/Invoice/Cheque** | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | **Bills Discounting (Bills of exchange including cheques)** | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | **Documentary Collection - Export** | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | **Documentary Collection - Import** | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | **Outward Bills for Collection (clean collections & TCs)** | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | **Inward Bills for Collection** | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | **Local Currency Transactions** | | **Local Currency Transactions** |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | **Foreign Currency Transactions** | | **Foreign Currency Transactions** |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | **Statements** | | **Statements** |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | **Cheque Books Issuing** | | **Cheque Books Issuing** |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | **Standing order** | | **Standing order** |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | **Insufficient funds/effects not cleared** | | **Insufficient funds/effects not cleared** |
| | Effects not cleared | **ITEM REMOVED** | **ITEM REMOVED** |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | **Other services/charges** | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | | **Signature:** |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | **Chief Operating Officer** | | **Country Chief Finance Officer** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |

**Disclaimer: All fees are VAT exclusive.**

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.09.2020

### Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Sep-20 | Robo Mwaka ya 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,632 | 3,016 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,479 | 7,339 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 23,924 | 78,351 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,188 | 5,091 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 33,654 | 28,711 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 47,374 | 51,687 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,194 | 4,123 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,381 | 1,449 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **123,826** | **179,767** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 21,460 | 56,439 |
| 18 | Amana za Wateja | 65,691 | 85,521 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 3,956 | 6,023 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 928 | 1,232 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 6,015 | 6,766 |
| 27 | Dhima Nyingine | 886 | 899 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **98,937** | **156,880** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **24,889** | **22,887** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (40,582) | (40,582) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 4,948 | 2,945 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **24,889** | **22,887** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 859,823 | 848,304 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,097 | 4,144 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 225 | 225 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 20% | 13% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.59% | 8.0% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68% | 57% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 38% | 29% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85% | 88% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -24% | -22% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -31% | -17% |

Katika kipindi cha robo mwaka iliyoisha benki ilitozwa faini ya fedha za kitanzania millioni tano kwa kukiuka kifungu namba 3.1 cha "Foreign Exchange Circular No. 6000/DEM/EX.REG/58" ya tarehe 24 mwezi wa Septemba mwaka 1998 katika utekelezaji wa mikopo itolewayo nje ya nchi.

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-20 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,085 | 3,895 | 10,937 | 8,092 |
| 2 | Gharama za Riba | (759) | (1,344) | (3,613) | (2,932) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,326** | **2,551** | **7,324** | **5,160** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | (181) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **3,553** | **2,640** | **8,515** | **6,752** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 458 | 290 | 1,055 | 1,037 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 3,081 | 2,331 | 7,410 | 5,622 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 13 | 18 | 50 | 92 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,858)** | **(3,248)** | **(10,837)** | **(10,307)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,581) | (1,603) | (4,961) | (4,709) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (361) | (5) | (662) | (947) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,916) | (1,640) | (5,215) | (4,651) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **2,021** | **1,942** | **5,002** | **1,423** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (18) | (18) | (55) | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,003** | **1,924** | **4,947** | **1,423** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **2,003** | **1,924** | **4,947** | **1,423** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 115 | 117 | 115 | 117 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 319 | 306 | 787 | 226 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 | 4 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.32% | 1.07% | 3.26% | 0.27% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 8.38% | 8.41% | 20.71% | 3.72% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 58.12% | 49.71% | 55.71% | 60.79% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.76% | 1.61% | 5.55% | 1.60% |

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Mussa Kitambi<br>**Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wakubwa** | *Imesainiwa* | *23rd October 2020* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | *Imesainiwa* | *23rd October 2020* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | *Imesainiwa* | *23rd October 2020* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *23rd October 2020* |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *23rd October 2020* |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Sep-20 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **2,003** | **1,924** | **4,947** | **1,423** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 121 | 256 | 121 | 82 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 4,313 | (7,785) | 4,313 | (885) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (56,877) | (38,761) | (56,877) | (70,401) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 54,428 | 10,701 | 54,428 | (46,722) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (12) | (540) | (12) | (235) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (71) | 1,342 | (71) | (583) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **3,904** | **(32,862)** | **6,848** | **(117,322)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (56) | (120) | (56) | (225) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(56)** | **(120)** | **(56)** | **(225)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 29,916 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **29,916** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **3,848** | **(32,982)** | **6,793** | **(87,631)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 74,812 | 107,794 | 107,794 | 239,669 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **78,660** | **74,812** | **114,587** | **152,038** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2020 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (40,582) | - | - | - | 19,942 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 4,948 | - | - | - | 4,948 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (35,635) | - | - | - | 24,889 |
| Mwaka uliopita 2019 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (42,568) | - | 402 | - | 18,358 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 2,009 | - | - | - | 2,009 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | | | - | | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (40,559) | - | 402 | - | 20,367 |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

# Vijana watakiwa utulivu uchaguzi mkuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA nchini wametakiwa kuwa watulivu katika kipindi chote cha uchaguzi mkuu 2020, na kuacha kutumika na wanasiasa ili kufanya maandamano yatakayosababisha uvunjifu wa amani.

Mwenyekiti wa wamachinga wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Baraka Mrisho, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi mkuu 2020, unaotarajia kufanyika kesho.

"Nawaomba vijana wenzangu, kipindi hichi tuwe watulivu na tujitokeze kwa wingi kupiga kura kwa wale wenye sifa ya kupiga kura kumchagua mtu mwenye tija na nchi yetu na tuondoe itikadi za vyama vyetu," alisema Mrisho.

Pia, alisema kuwa hakuna kitu muhimu nchini kama amani na utulivu kwani kama vijana watashiriki katika kuliharibu taifa litaingia katika machafuko.

Alisema, vijana wanao wajibu wa kuhahakisha kuwa amani iliyopo nchini inalindwa kwa hali na mali, hivyo wakati huu wa uchaguzi mkuu wanayo sababu ya kuwa watulivu na kuacha kutumika kufanya maandamano.

"Vijana tusidanganyike na maneno ya wanasiasa wanayoyatumia katika kipindi hicho cha uchaguzi mkuu, sisi wenyewe tunayo macho tunaona tumchagiue mtu kwa kazi zake na siyo maneno matupu," alisema Mrisho.

Aliwataka, viongozi wa dini nchini kuendelea kuwahubiria umuhimu wa kuitunza amani kwa kuwa ndiyo kila kitu kwa taifa.

"Kama walivyofanya maombi kuombea kuondoka kwa mlipuko wa virusi vya corona nchini ndivyo ambavyo wanatakiwa kuombea amani yetu iendelee kudumu kwani sisi Watanzania hakuna hata anayejua kuchimba handaki," alisema.

Vilevile, aliitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza matokeo kwa wakati, ili kuondoa vurugu zinazoweza kujitokeza.

Kadhalika Mrisho alisema kuwa mawakala wa vyama vya siasa wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kulinda amani ya nchi, na kutenda haki kwa maslahi ya taifa na siyo yao binafsi.

Aidha, aliwaonya vijana kuacha kujihusisha na vitendo vya kuuza vitambulisho vyao vya kupiga kura kwa wanasiasa, kwani ni kosa kisheria na wanajinyima haki yao ya kikatiba ya kuchagua kiongozi.

"Wanasiasa wanaweza kufanya lolote kwa kununua vitambulisho vya kupiga kura kwa maslahi yao binafsi ya kutaka kushinda katika nafasi wanazozitaka," alisema.

Mwenyekiti wa umoja wa vijana wa soko la Sabasaba, jijini hapa, Emmanuel Mtega, alisema vijana wanatakiwa kujitambua nini wanatakiwa kufanya katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

Mtega, alisema kuwa kijana kupewa fedha na mwanasiasa isiwe sababu ya yeye kuchagua kiongozi asiye na sifa.

"Vijana tunatakiwa kuwa makini na wanasaiasa wanaotutumia kwa maslahi yao binafsi kwa kufanya kitu sahihi, kumchagua kiongozi bora bila ya kudanganywa na mtu," alisema Mtega.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Zuwena Omary, akimkabidhi Gift Lyimo cheti cha kuhitimu darasa la saba kwenye mahafali ya tisa ya Shule ya Awali na Msingi New Light iliyopo Mji Mdogo wa Mirerani. **PICHA: GIFT THADEY**

# UVCCM wawacharukia wanaobeza kazi za JPM

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UMOJA wa Vijana wa CCM (UVCCM) mkoani Shinyanga, umewataka wananchi kuwapuuza wale ambao wanabeza mambo yaliyofanywa na Rais John Magufuli.

Mwenyekiti wa UVCCM mkoani Shinyanga, Baraka Shemahonge, alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa kampeni wakati akimnadi mgombea udiwani wa Ndembezi Manispaa ya Shinyanga kupitia CCM, David Nkulila.

Alisema baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzani wamekuwa wakitumia majukwaa ya kampeni vibaya, kwa kubeza maendeleo ambayo yamefanywa na Rais Magufuli katika kipindi chake cha utawala wa miaka mitano na kuwataka wananchi wayapuuze maneno hayo.

"Natumia fursa hii kuwataka Watanzania kuwapuuza watu ambao wanabeza maendeleo yaliyofanywa na Rais Magufuli, 'wanasema eti amefanya maendeleo ya vitu na siyo ya watu', huko ni kukosa sera za kuwaambia wananchi kwenye mikutano yao ya kampeni," alisema Shemahonge.

Pia aliwataka wananchi kesho wajitokeze kwa wingi kwenda kupiga kura, na kumchagua tena Rais Magufuli, kwa miaka mitano mingine na kuwaletea maendeleo, pamoja na kukamilisha miradi mikubwa ambayo aliianzisha.

## Msimamizi wa uchaguzi ahimiza amani, utulivu

**Na Mohab Dominick,** MBOGWE

MSIMAMIZI wa uchaguzi Jimbo la Mbogwe mkoani Geita, Elias Kayandabila, amewaomba wananchi wa jimbo hilo na taifa kwa ujumla kuilinda amani iliyopo kwa kutosababisha vitendo vya uvunjifu wa amani kesho.

Aidha, msimamizi huyo amesema kuwa iwapo vyama ama wananchi wenyewe wakiwa na malalamiko wawasilishe katika ofisi ya msimamizi huyo, ili kutatuliwa changamoto zao.

Msimamizi huyo wa uchaguzi Jimbo la Mbogwe, Elias Kayandabila, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Kayandabila akizungumzia suala la maandalizi ya uchaguzi mkuu alisema kuwa asilimia 98 yamekamilika na kwamba wanaendelea kupokea vifaa mbalimbali vya uchaguzi, huku akisema kuwa vyama vyote vimepata mawakala, na kuongeza kuwa kama msimamizi wa uchaguzi hajapata malalamiko yoyote juu ya suala hilo.


"Kwanza niishukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa sababu tunakimbilia mwisho wa zoezi la uchaguzi na hadi sasa kwa maandalizi asilimia 98 ya maandalizi hayo tayari yamekamilika, tulianza kwanza kwa mafunzo ya wasimamizi wote wa uchaguzi yamekamilika," alisema Kayandabila na kuongeza:

"Lakini tumepokea vifaa na hadi sasa vifaa vya tume vinaendelea kuletwa na vichache tu bado havijafika vipo njiani na mafunzo ya wasimamizi katika kata yamekamilika."

Pia alisema wasimamizi wa uchaguzi wa vituo wameshapatikana baada ya nafasi kutangazwa na kwamba wanatarajia kuwa na wasimamizi zaidi ya 1,200.

Pia msimamizi huyo alisema kuwa jimbo hilo linajumla ya vituo 413 vya kupigia kura na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi vituoni ili kuchagua viongozi watakaoona wanafaa kuwaletea maendeleo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 27, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

## Vyama vinapohangaikia mfumo mpya elimu ni hitaji au hisia tu?



Ukurasa 12

**Wanavijiji waambiwa misitu ni kila kitu ikiwamo pensheni**



Ukurasa 14

Mkoa kinara mimba, ndoa utotoni waerevuka

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Wanafunzi wasaka ajira, kuna lulu usafiri wa anga

INGAWA sekta ya usafirishaji wa anga nchini, inakua kwa kasi baada ya serikali kuipa msukumo mpya ikiwamo kununua ndege za kisasa, inaelezwa kuwa inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa wataalamu.

Changamoto hiyo inatokana na kukimbia masomo ya sayansi ambayo ni kigezo kikubwa cha wale wanaotaka kujiunga na masomo hayo ya kuhudumia usafirishaji wa anga.

Upungufu huo unaonekana kwenye mafundi wa kutengeneza ndege ambayo imeharibika yaani (Aircraft Maintenance Engineers) na wafanyakazi wanaotakiwa kutoa maelekezo kwa rubani kabla hajaenda kwenye chumba chake cha kuendeshea ndege yaani (flight dispatchers, anasema Mkuu wa Chuo cha Regional Aviation College, Hulka Omar.

Ili kutatua changamoto hii, serikali haina budi kuwekeza zaidi kwenye vyuo vinavyotoa mafunzo ya usafirishaji wa anga bila kujali ni vya umma au binafsi ili kuzalisha watalaamu wengi zaidi, anasisitiza.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Chuo cha Regional Aviation College, kilichopo uwanja wa ndege wa Dar es Salaam, anasema ili kutatua changamoto hizo chuo chao kimeanza kutoa kozi ya 'Aircraft Maintenance Engineering (AME) inayofundisha wataalamu wa kutengeneza ndege.

Aidha, kuna kozi za flight dispatch na flight operations' zinazowafunza wataalamu wa kutoa maelekezo kwa rubani kabla ya kuingia kwenye chumba chao na kuanza kuendesha ndege.

Anasema chuo kina wakufunzi 15 waliosoma katika vyuo vya nchi za Canada, Pakistan, Uingereza, China, Uganda na Scotland ambao wanafundisha kozi mbalimbali.

Akielezea kozi ya Aircraft Maintenance Engineering (AME) anasema inachukua miaka mitatu ambayo ni kuwaandaa au kuwatengeneza mafundi wa kutengeneza ndege zlizoharibika.

Mpaka sasa zaidi ya wahitimu 170 wamehitimu kozi hii na wengi wao wameajiliwa kwenye mashirika ya Precision Air, Air Tanzania, Coastal Airlines, Auric Air na mengine ya Dubai.

"Ingawa tumeanza kutoa mafunzo kwa wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali, kuna mahitaji makubwa ya wataalamu wa kozi hizi kwa asilimia 60," anasema Omar.

Anawakaribisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali kujiunga na kozi hizo kwa sababu ajira zipo kwa wingi kwa vile wahitimu wanapata kazi kwenye mashirika ya ndege ya ndani na nje ya nchi kama Nigeria, Kenya na Dubai.

"Tunakaribisha wanafunzi kuanzia kidato cha nne hadi chuo kikuu, vigezo ni ufaulu kwenye masomo ya sayansi ikiwamo fizikia, kemia, hisabati kwa kupata alama D nne na kuendelea," Omar anasema.



Mhandisi ndege aliyejifunza kozi ya kutengeneza ndege akiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

### MAFUNDI WA NG'AMBO

Omar anaeleza kuwa kabla ya kuanzisha kozi hizo, mafundi wengi wa kutengeneza ndege zilizoharibika walitoka nje hasa Uingereza, Ujerumani, Marekani na Ufaransa.

Mbali na hilo mashirika mengi ya ndege yalikuwa yanatumia fedha nyingi kugharamia wataalamu hao.

"Tumeamua kuanzisha kozi hii baada ya kugundua kuwa mashirika mengi hayana mafundi wazawa wa kutengeneza ndege hizo," anaongeza Mkuu wa Chuo.

Akielezea kozi ya 'flight dispatch au flight operations' anasema hii ni kozi ya miezi sita na imeanzishwa mwaka 2014 baada ya kuona kuna upungufu wa wafanyakazi wanaotakiwa kutoa maelekezo kwa marubani kabla hawajaenda kwenye chumba chake cha kuendeshea ndege.

"Kabla rubani hajakwenda kwenye chumba chake cha kuendeshea ndege, lazima apate taarifa za kumwezesha katika safari yake yote awapo angani muda wote na aweze kusafiri kwa usalama kutoka kwa 'flight dispatcher'." Anasema.

Omar anaelezea taarifa hizo kuwa ni kama vile hali ya hewa, jinsi mpangilio wa mizigo utakavyowekwa kwenye ndege na umbali wa kuruka kutoka usawa wa bahari.

Mara nyingi taarifa hizi zinamsaidia rubani kujua kiasi gani cha mafuta kinatakiwa kuwekwa kwenye ndege na kasi ya kuondokea uwanjani.

Mpaka sasa zaidi ya watu 350 wameshahitimu kozi hiyo anasema kuongeza kuwa wengi hufanya kazi katika viwanja vyote vya ndege duniani hasa kwenye mashirika yanayotoa huduma kama vile Swissport na United Aviation Services (UAS).

"Hivi sasa tunakaribisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini waje kusoma kozi ya flight dispatch katika chuo chetu kwa sababu ajira zipo nyingi baada ya kuhitimu masomo na ajira ni za uhakika," anasema Omar.

Ufaulu unaotakiwa ni masomo ya sayansi ikiwamo jiografia, fizikia, hisabati na hata wenye kiwango cha alama D wanakubalika bora ziwe nne na kuendelea.

"Kozi hii haikuhitaji mpaka uwe na shahada, kuanzia kijana wa kidato cha nne anaweza kujiunga na chuo," anahimiza mkuu huyo wa chuo.

### MANUFAA YA KOZI

Akielezea faida za kozi hiyo anasema mwanafunzi anayesoma mafunzo hayo ana faida hizo: "Kwanza anapata cheti cha kimataifa ambacho kinatambulika ndani na nje ya nchi. Pili anaajiriwa popote duniani na mashirika ya ndege."

Aidha, anasema mwaka 2020/2021, chuo kina mpango wa kuanza kutoa kozi nyingine kama kozi ya wafanyakazi wa ndani ya ndege (cabin crew), kozi ya bidhaa hatari (dangerous goods) ili wazitambue kabla hazijaingizwa kwenye ndege.

Mbali na hilo pia wanatarajia kutoa kozi ambazo zipo chini ya Umoja wa Mashirika ya Ndege Duniani (IATA) baada ya kupata usajili kamili wa IATA.

**INAENDELEA UK.13**

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Wanavijiji waambiwa misitu ni kila kitu ikiwamo pensheni



Mgombea ubunge John Sallu (kulia), akimwonyesha ofisa TFCG, Revocatus Njau, mti wa utafiti shambani kwake akiwa na lengo la kusaidia kupata miche bora. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

MISITU ni mali, ndiyo kauli mbiu ya wakazi wa Handeni mkoani Tanga ambao wanaanza kufunzwa mbinu za ujasiriamali wa misitu zinazolenga kuwaongezea kipato ikiwamo cha kujikimu uzeeni na pia kunusuru ardhi yao isiwe jangwa.

Mgombea ubunge wa Handeni (CCM) John Sallu, anaanza kufanya kampeni kuhamasisha wananchi katika jimbo hilo kupanda miti kama njia mojawapo ya kujiongezea kipato na kupunguza ukataji misitu unaochangia kuharibu vyanzo vya maji.

Sallu mwenye shamba la eka tano lenye aina mbalimbali za miti kutoka mataifa mengine duniani kama Brazil, Australia, Afrika Kusini na Zimbabwe, anasema imepandwa kwa ajili ya utafiti na baada ya miaka minne wataangalia ni ipi bora ili waitunze kupata kipato.

Mgombea ubunge anasema hayo hivi karibuni alipokutana na wadau wa misitu kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) pamoja na wanahabari, waliotembelea shamba lake la miti la ekari tano lilipo Handeni.

"Hadi sasa nimefanya kampeni katika kata na vitongoji mbalimbali wilayani Handeni huku nikiwahamasisha wananchi angalau kila kaya kutenga eka moja kupanda miti na kuhifadhi misitu iliyo katika ardhi ya vijiji," anasema.

Anasema ameamua kuhamasisha wananchi kupanda miti kwa sababu ni chanzo cha mapato yanayotokana na matunda, mkaa, mbao na kuni.

> "Viongozi wa siasa lazima tusaidie juhudi za serikali na watu katika kulinda misitu, kupunguza ukataji wa misitu ili kunusuru nchi na athari za mabadiliko ya tabia nchi na nchi kuwa jangwa.

Anasema Handeni yenye vijiji 91, kata 21 na vitongoji 770, asilimia 90 ya wakazi wake wanategemea misitu kwa ajili ya kuni, biashara ya mkaa na mbao kwa ajili ya shughuli za ujenzi, hata hivyo licha ya mali hizo kutoka katika misitu iliyo katika ardhi ya vijiji bado haijahifadhiwa kisheria.

Anawataka wakulima kupanda miti kwa sababu itawatunza hasa uzeeni, "miti itakusaidia hata ukiumwa unaweza kwenda ng'ambo kujitibu," anasema Sallu.

Hii ni kampeni ambayo imebuniwa kusaidia serikali za vijiji kunusuru takribani hekta milioni 17.6 za misitu ambazo bado hazihifadhiwa kisheria, ikiwa ni karibu asilimia 80 ya hekta milioni 22 za misitu iliyo katika ardhi ya vijiji ambayo inaharibiwa na shughuli za kilimo, uchomaji mkaa, mbao, mifugo.

Madhumuni ya ziara hiyo yalikuwa kuwaonyesha aina za miti ambayo imepandwa katika shamba hilo kwa ajili ya ufatiti ili kuona ni jamii ipi itastawi katika wilaya ya Handeni kwa ajili ya mbao, mkaa na matunda kulingana na mazingira na hali ya hewa.

"Mwananchi akiamua kupanda miti kwenye eka moja katika shamba lake anaweza kupata Sh. milioni 20 na hii inategemea aina ya miti aliyopandwa," anasema.

Anasema ameamua kujikita katika kampeni hii baada ya kugundua kuwa uhifadhi wa misitu na upandaji wa miti ni chanzo cha mapato, unapunguza umaskini, jangwa, inalinda vyanzo vya maji, inachangia maendeleo ya uchumi ikiwamo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mbali na hilo, misitu iliyopandwa shambani inaweza kusaidia watu kupambana na njaa, utapiamlo, kuboresha soil fertility, kuvuna matunda hata viungo.

"Viongozi wa siasa lazima tusaidie juhudi za serikali na watu katika kulinda misitu, kupunguza ukataji wa misitu ili kunusuru nchi na athari za mabadiliko ya tabia nchi na nchi kuwa jangwa," anasema.

## KUPATA MICHE

Anasema katika kampeni hiyo wananchi watapewa miche ya miti ili kupanda mashambani kwao na maeneo mengine ambayo yameharibiwa kwa ajili ya ukataji misitu ili kupunguza umaskini, njaa na ukataji wa misitu katika ardhi ya vijiji.

"Nitashirikiana na wadau mbalimbali kutoa miche ya miti kwa ajili ya upandaji wa miti na pia nitawapeleka wanakijiji kwenye shamba langu la misitu ya asili ili waweze kuona na kujifunza kwa sababu kuona ni kuamini, nataka wajifunze kitu nilichofanya katika shamba langu baadaye waende kufanyia kazi katika mashamba yao," anasema mgombea huyo.

Mbali na hilo pia anaahidi kushirikiana na wadau wengine kama Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), MCDI ili kusaidia vijiji kutengeneza mpango wa uvunaji wa misitu katika maeneo yao na kusimamia uvunaji endelevu katika misitu iliyo katika ardhi ya vijiji.

## MAJI HANDENI

"Nikichaguliwa kuwa mbuge, nitasaidia wananchi kutimiza malengo yao katika shughuli za upandaji wa miti na uhifadhi wa misitu, ili kulinda vyanzo vya maji. Nitahakikisha suala la maji na misitu vinapewa kipaumbele ili kusaidia wananchi wa Handeni kuondokana na tatizo la maji na uharibifu wa misitu," anasema Sallu.

"Maji ni muhimu katika kuleta maendeleo endelevu, hivi sasa upatikanaji wa majisafi na salamu ni tatizo kubwa linalowakabili wananchi katika Wilaya ya Handeni.

Anawataka kinamama na watoto wa kike wamekuwa wakitembea mwendo mrefu kwenda kuchota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

"Kama unavyofahamu maji yanahitajika kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo, viwandani, uzalishaji wa umeme, upandaji wa miti na hata katika sekta ya utalii kwa ajili ya wanyamapori. Na mpaka sasa jumla ya vijiji 91 vya wilaya ya Handeni vina changamoto ya upatikanaji wa majisafi na salama," anasema mgombea huyo.

Ofisa Mawasiliano na Uragibishi wa Shirika la TFCG, Revocatus Njau, alisema kuwa ili kunusuru misitu ambayo bado haijahifadhiwa kisheria katika ardhi ya vijiji, TFCG kwa kushirikiana na wadau wengine wameanzisha kampeni ya "misitu ya hifadhi kwa kila kijiji".

Lengo ni kunusuru tarkribani hekta milioni 17.6 za misitu ambazo bado hazijahifadhiwa kisheria.

"Ikiwa ni karibu asilimia 80 ya hekta milioni 22 za misitu iliyo katika ardhi ya vijiji na hii ni muhimu kwa sababu kila mwaka zaidi ya hekta 460,000 za misitu hasa ambayo bado haijarasimishwa hufyekwa na kuongeza zaidi ya tani milioni 44 za hewa ukaa kwenye anga la dunia, hali inayochangia mabadiliko ya tabia nchi," anasema.

Anasema kauli mbiu ya kampeni hiyo ni: "Kila kijiji chenye msitu wa asili katika ardhi yake kina haki ya kuanzisha, kumiliki na kusimamia Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwa manufaa ya sasa na ya kizazi kijacho," anasema.

Pia kupitia kampeni hii TFCG inahamasisha kila kijiji chenye msitu wa asili ambao haujarasimishwa kiutenge kuwa msitu wa hifadhi wa kijiji na kuusimamia kikamilifu.

"Tayari tumeishatembelea katika kijiji cha Madebe na Kang'ata katika Wilaya ya Handeni kwa kuanzia na baadaye tutakwenda katika vijiji sita vilivyopangwa ili wananchi waweze kutenga maeneo ya misitu ya hifadhi ya vijiji na kujikita katika usimamizi shirikishi wa misitu vijijini kwao," anasema.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Vyama vinapohangaikia mfumo mpya elimu ni hitaji au hisia tu?

SUALA la mfumo wa elimu unaoendana na mahitaji ya kimaisha baada ya kuhitimu limetawala hisia za wataalamu na viongozi tangu uhuru hadi sasa.

Ni mwaka 1967 ambako Mwalimu Julius Nyerere aliliinua suala hilo kuwa la kiitikadi akichapisha andiko la elimu ya kujitegemea, akieleza dhamira ya elimu inayomwezesha mwanafunzi kuishi vyema akiwa kijijini.

Aliona hitaji la kazi mijini linawakumba wote wanaomaliza darasa la nane na saba baadaye na kama hawafaulu kupata kazi mijini pale wasipochaguliwa kuingia sekondari, wanakuwa wamefeli maisha.

Tafakuri ya suala hilo imekuwa ikibadilika na hali kuwa tofauti muda unavyozidi kwenda, kwani mwaka 1967 Mwalimu alikuwa anaangalia wale wanaomaliza shule za msingi, baadaye wakasahaulika.

Miaka ya 1980 na 1990 mijadala ililenga zaidi wanaomaliza sekondari na kuanzia 2010 hadi sasa mwelekeo wa tafakuri ni kwa wanaomaliza vyuo na vyuo vikuu, lakini kimsingi hoja za awali zinaendelea kimfumo.

Ilivyo leo, pengine kupata kazi ya kuajiriwa ni kielelezo cha kufaulu katika maisha, lakini siyo kila kitu. Hakuna mbinu za wazi za kuwezesha watu wafaulu katika biashara na hasa kushauri mtu huyu au yule ajiunge na biashara gani, lakini eneo hilo wapo wanaojiajiri na kuajiriwa au kufaidika kwa kutoa huduma za aina tofauti.

Hilo linakuwa halizungumziwi kwani ni suala la mtu kujituma nafasi inapotokea au upenyo fulani na hakuna taaluma inayoamua.

Kwa maana hiyo kuna ufa au utengano wa wazi kati ya kile kinachoelezwa katika majukwaa na ukiangalia kwa karibu hali halisi, unakuta kuwa lengo la Mwalimu kisiasa lilikuwa ni kufuta dhana kuwa ambao hakusoma sekondari au zaidi 'wameshindwa kimaisha.'

Alitaka vijana na hasa wazazi wa watoto katika shule za msingi waangalie elimu ya msingi kama andalio tu.



Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

Fikra hiyo ya Mwalimu ni kama vile ilitimia baadaye ila katika mazingira tofauti na ilivyotazamiwa, kwani jawabu la kupatikana 'elimu ya kujitegemea' halikuwa kubadili mawazo kuacha kufikia kazi za kuajiriwa na kujikita kijijini.

Kwa miaka 10 hadi 15 iliyofuata hali hiyo iliendelea huku mazingira yakibadilika, elimu ya msingi ikiwa siyo tena kigezo cha kutafuta kazi, labda za huduma kama kufagia, si huduma za ofisi kama ukarani na hata mapokezi.

Vijana waliomaliza shule za msingi wakawa watu wa kawaida na wakihamia mijini wanatafuta maisha.

Bado katika miji kuna watu ambao wanajua kusoma na kuandika kwa taabu na yako maeneo hata Ulaya wapo wakazi wa viunga vya jiji kubwa hajui kusoma na kuandika.

Hata hivyo ilikuwa ni miongoni mwa wahamiaji mfano Ufaransa, ambako watu walikuwa miaka ya 1970 wanaingia na familia zao, mama anakuwa hajui kusoma na anabaki nyumbani.

Ni hali iliyokuwa imeanza kusambaa kutokana na uwezo mdogo wa serikali kujenga shule na mwaka 1974 ukaja mpango wa elimu kwa wote (UPE- Universal Primary Education) ambao ulikuwa na kipengele cha kufundisha walimu (hata waliomaliza shule za msingi) kwa haraka wafundishe wengine.

Ndiyo hapo viwango vilianza kuporomoka kwani suala lilikuwa ni 'kufyatua' walimu idadi iliyopangwa na kuandikisha watoto idadi iliyokwisha pangwa na hapakuwa na suala la kurudi nyuma hadi vifaa na uwezo wa kufundisha au kuchukua tu waliomaliza sekondari na kufaulu. Kuanzia wakati huo serikali imekuwa ikivutana na wanataaluma kuhusu ubora wa elimu nchini, huku baadhi yao wakihisi kuwa tatizo ni lugha ya kufundishia, kwani matumizi ya Kiingereza yaliporomoka miaka hiyo.

> Vijana waliomaliza shule za msingi wakawa watu wa kawaida na wakihamia mijini wanatafuta maisha.

Hata hivyo mfumo wa elimu ukalazimika kubakiza nafasi ya Kiingereza, ili kutojitoa katika elimu kimataifa.

Ila mazingira hayo hayaleti kikamilifu hitaji la kubadilisha mfumo wa elimu nchini, kwa mfano ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanaweza kushindania kazi za kimataifa, kama alivyosema mgombea urais mmojawapo.

Ni wazi kuwa wale wanaosoma katika shule zinazofundishwa kwa Kiingereza watakuwa na nafasi zaidi katika eneo hilo la lugha, lakini wanaosoma kwingineko mara nyingi wanawafikia katika ngazi ya elimu ya sekondari.

Hata shule za sekondari za kata, ambako huwezi kukuta mwanafunzi aliyetokea 'English medium' zimekuwa zikishika namba za juu kwa ufaulu mitihani ya kidato cha nne.

Ni kwa njia hiyo pia ambapo unaweza kuangalia suala la kujiajiri ambalo limewekewa mkazo wa kushangaza katika mijadala ya elimu kwa jumla, wakati siyo jawabu.

Kimsingi suala la ajira linabakia na hili la kujiajiri ni la kupanuka kwa biashara, hivyo mtu akipewa mafunzo kuhusu biashara anaelewa zaidi kinachotokea kuliko anayejifunza kwa kuingia mtaani.

Tofauti ni kuwa shughuli za kibiashara zinaendana na hulka au vipaji vya watu na siyo masomo yao na kwa maana hiyo andiko la Mwalimu cha elimu ya kijitegemea linaendelea kufanya kazi, kuwa kusoma hadi sekondari au chuo cha kati au cha elimu ya juu ni matayarisho ya kumudu maisha, ambayo yanaweza kuwa ajira, ushiriki wa huduma fulani kama mtu anayejitegemea kwa mfano wanamichezo au wasanii maeneo tofauti.

## Wanafunzi wasaka ajira, kuna lulu usafiri wa anga

**INATOKA UK.11**

"Kozi hizo ni kama airport operations, air cargo, air fare and ticketing," anasema na kuongeza kuwa umuhimu wa kozi ya airport operations ni wa kipekee na imeandaliwa kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa shughuli zote katika kiwanja cha ndege."

"Kwa mfano wafanyakazi wanaofanya kazi katika Shirika la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) ni wahitimu wa kozi hiyo," anaongeza.

Kwa wanafunzi wanaohitaji kusoma kozi hizo tayari chuo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).

"Ingawa sekta ya anga inakuwa kwa kasi sana, lakini bado haiendani na hali halisi kwa sababu wataalamu wanaohitajika kufanya kazi eneo hili ni wachache mno," anasema.

**WASOMI WAZUNGUMZA**

Fundi wa kutengeneza ndege katika Shirika la Precision Air, Alisen Majja, akizungumza na Nipashe, anasema hivi sasa kuna wanafunzi wengi wanapenda kusoma kozi hizi, lakini hawana ada.

Mbali na hilo, chuo na uongozi wa mashirika ya ndege inabidi waanzishe ushirikiano ambao utakuwa rahisi kwa wanafunzi kujitolea au kufanya kazi ili kukuza sekta ya anga.

Anawaomba wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini waliofaulu masomo ya sayansi kwenda kusoma katika chuo hicho kwa sababu chuo kinatambulika na NACTE na tayari kimesajiliwa na NACTE, ili kusaidia Tanzania kupata wataalamu wengi zaidi katika sekta ya anga.

"Nilianza kozi ya aircraft maintenance engineering mwaka 2014 na kuhitimu Novemba 2017, baada ya hapo niliajiriwa na Precision Air," anasema Majja.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Taleck (katikati), akizindua mpango mkakati wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Kulia ni Mkurugenzi Mkazi wa UNFPA, Dk. Willfred Ochani na Mkurugenzi Mkazi KOICA, Kyucheol Eo (kushoto). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mkoa kinara mimba, ndoa utotoni waerevuka

MIMBA na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga zinatajwa kuwa zinachochewa na jamii kuamini kuwa mabinti hawana thamani nyingine mbali na kuongeza utajiri kwa familia zao.

Ndoa hizo zinawakwamisha watoto wa kike kutimiza ndoto zao kwenye elimu, kwa vile zinawazuia kusoma kuanzia shule za msingi hadi sekondari.

Ili kuwanusuru wasichana hawa, mkoa umeweka mkakati wa ulinzi imara wa mwanamke pamoja na mtoto kumaliza matukio ya ukatili dhidi yao ili waweze kutimiza ndoto zao huku wakiepuka ujauzito na kuozeshwa utotoni kwa tamaa za wazazi wanaotaka pesa na mifugo.

Mkoa unalimaliza tatizo hilo kupitia mpango mkakati wa miaka mitano wa kutokomeza ukatili ndani ya jamii dhidi ya wanawake na watoto, ulioanza mwaka huu hadi 2025.

Aidha, itakuwa ndiyo dira ya mashirika yasiyo ya kiserikali katika kutekeleza miradi ya kupambana na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, takwimu za kitaifa za mwaka (2012), zinaonyesha kuwa Shinyanga inaongoza kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora 58 na wa tatu ni Mara kwa asilimia 55, ambapo wanafunzi wamekuwa wakipewa mimba na kuolewa chini ya umri wa miaka 18 na kuzima ndoto zao.

### ATHARI ZA CORONA

Takwimu za miezi mitatu ndani ya kipindi cha likizo ya corona, zilizotolewa na

> Shinyanga ni ya kwanza nchini, kuwa na mkakati kama mkoa kupambana na kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

mratibu wa mpango mkakati wa serikali wa kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) Tedson Ngwale, wanafunzi 101, walipewa ujauzito na kuacha masomo.

Serikali ya Mkoa wa Shinyanga imetengeneza mpango mkakati wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ili kumaliza matukio ya wanafunzi kupewa ujauzito pamoja na kuozeshwa utotoni.

Mkuu wa Mkoa Zainab Taleck, anasema Shinyanga ni ya kwanza nchini, kuwa na mkakati kama mkoa kupambana na kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Anasema baada ya kuona kuna kushamiri matukio hayo ya ukatili, mkakati huo ukaandaliwa ili uwe mwarobaini wa kutokomeza matukio ya ukatili likiwamo tatizo la mimba na ndoa za utotoni.

"Mpango mkakati huu ambao tunauzindua mkoani Shinyanga, utakuwa ni mwarobaini wa kutokomeza matukio ya ukatili tunataka kuwapo na usawa wa kijinsia, pamoja na watoto wote wa kiume na wa kike wapate elimu sawa na kusiwepo tena na matukio ya mimba wala ndoa za utotoni," anasema Zainabu.

### YATAKAYOFANYIKA

"Kazi ambazo zitafanywa kwenye mpango huu, ni kusimamia ipasavyo sheria na kanuni zinazolinda haki na ustawi wa wanawake pamoja na watoto, kuendesha kampeni za ujenzi wa nyumba salama, kuelimisha jamii kuhusu malezi bora, kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa kamati za ulinzi wa mtoto kuanzia ngazi ya kijiji.

Nyingine ni kuanzisha vituo vya kutosha vya huduma ya mkono kwa mkono (one stop center), kuhamasisha jamii kushiriki shughuli za kiuchumi na kujiletea maendeleo, kuwezesha wanawake kiuchumi, pamoja na kupambana na mila na desturi kandamizi zinazokwamisha," anaongeza.

Aidha, anatoa wito kwa viongozi serikali ngazi zote, kuusoma mkakati huo na kuulewa, ili kila mmoja awajibike katika eneo lake na kufanya kazi wa ushirikiano na kufikia malengo ambayo wamejiwekea ifikapo 2025.

Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Afya Sifuni Msangi, anaipongeza Shinyanga kwa kuzindua mpango mkakati huo na kueleza kuwa ni utekelezaji wa mpango mkakati wa kitaifa wa kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto - MTAKUWWA ifikapo mwaka 2022.

Anasema mpango huo utakuwa ni dira nzuri kwa mkoa huo kuongeza kasi ya kupunguza matukio ya ukatili, na kufikia malengo ya serikali ya kupunguza matukio hayo kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

"Nimefanya ziara fupi kutembelea miradi ambayo inatekelezwa na Shirika la Investment Children and their Societies (ICS), wilayani Shinyanga, inayolenga kupambana na ukatili kwa wanawake na watoto na kubaini kuna vitu vinahitajika kufanyiwa kazi ili kumaliza ukatili huo," anasema Msangi.

"Baada ya kupitia mpango mkakati wenu huu nimeona umegusa vitu vyote ambavyo vinahitajika kufanyiwa kazi, hivyo ukitekelezwa ipasavyo Shinyanga haitakuwa na ukatili dhidi ya wanawake na watoto, wala mimba na ndoa za utotoni ambalo ni tatizo kubwa," anaongeza.

### WADAU WAUNGA MKONO

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA), Kycheol Eo, anasema Shinyanga ni miongoni mwa mikoa waliyoamua kuisaidia ili kuongeza nguvu ya kupambana kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Eo anasema ili kufikia hatua hizo KOICA kutoa Sh. bilioni 11 ili kutokomeza matukio hayo.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Willfred Ochan, anasema wanatekeleza mradi huo wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto mkoani Shinyanga kwa kushirikiana na KOICA.

Anasema kwa utafiti ambao waliufanya mkoani Shinyanga, kati ya wanawake 10, watano wameolewa kwa ndoa za utotoni na kwamba tatizo linalosababisha ni jamii kuwa na fikra potofu kuwa mtoto wa kike hana thamani.

"Kitu ambacho tunapaswa kukifanya ni kubadilisha mila na desturi kandamizi ndani ya jamii, ambazo ndio zimekuwa changamoto kubwa kuendelea kuwapo na matukio haya ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Tukifanikiwa hilo matukio haya yatabaki kuwa historia," anasema Ochani.

Mratibu wa mpango wa MTAKUWWA, Shinyanga Tedson Ngwale, anasema wameshaanza kuutekeleza mkakati huo kwa kufanya vikao katika kata zote mkoani humo, kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Anawataja kuwa ni watendaji wa kata, vijiji, maofisa maendeleo, ustawi wa jamii, dawati la polisi, pamoja na wajumbe wa kamati ya asasi hiyo ili kuweka mikakati ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni.

Anasema moja ya mikakati hiyo ni kutunga sheria ndogo pamoja na kuwekeana mikataba ambayo itakuwa ikiwabana watendaji wa vijiji na kata, kutokana na wao kuwa karibu zaidi na wananchi na huwa wanafahamu mipango yote ya mwanafunzi kutaka kuozeshwa ndoa ya utotoni, lakini hawatoi taarifa, na wakati mwingine hushiriki hata ndoa hizo.

"Tumegundua tatizo liko wapi. Mimba na ndoa hizi za wanafunzi kuendelea kuwapo kuna sababu na chimbuko lake ni uongozi kutowajibika kikamilifu upo uzembe unaofanyika katika kudhibiti vitendo hivi. Ndiyo maana tumeanza kulifanyia kazi ili kila mtu awajibike katika sehemu yake na kumaliza changamoto ya ukatili," anasema Ngwale.

Mtendaji wa Kata ya Jana, Kulima Mihambo, anasema licha ya kuwa na taarifa za mwanafunzi kupewa ujauzito ama kutaka kuozeshwa, wamekwamishwa kuwakamata wahusika kutokana na kuwapo wa uhaba wa polisi kwenye kata, pamoja na ukosefu wa fedha kwa ajili ya usafiri kwenda eneo husika.



# Wagombea waonywa vurugu uchaguzi mkuu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Huduma ya The Word Ministries, Damas Thadey, amewataka wagombea wa vyama vya siasa watakaoshindwa kwenye uchaguzi unaofanyika kesho kutokuwa chanzo cha kuwahamasisha wanachama wao kufanya vurugu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya ibada, Askofu Thadey alisema kwenye ushindani lazima kuwapo na mshindi na atakayeshindwa hivyo wagombea wanatakiwa kukubali matokeo watakayoyapata.

"Rai yangu kwao wapokee matokeo badala ya kuwahamasisha wanachama na wapenzi wa vyama vyao kuingia mitaani na kufanya vurugu na maandamano ambayo hayana tija na yatahatarisha uvunjifu wa amani," alisema.

Aliwataka wanachama na wapenzi wa vyama vya siasa kuacha mihemuko ya kushangilia matokeo yasiyo rasmi ambayo hayajatolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Askofu huyo alisema Tume hiyo iliyopewa mamlaka ya kutangaza matokeo si vinginevyo na kuwaomba wanachama wa vyama vya siasa kuzingatia hilo ili uchaguzi ufanyike kwa uhuru, haki na amani.

Aliwaasa vijana kutokubali kutumika kufanya vurugu kwenye maeneo wanayoishi ili waharibu uchaguzi huu. "Naviomba vyombo vya dola kamwe kutokubali kuona amani ikichafuliwa na baadhi ya watu," alisema.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge (katikati mwenye suti nyeusi), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 545 kwa vikundi vya wanawake, watu wenye ulemavu na vijana ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya Jiji la Dodoma, makabidhiano hayo yalifanyika jana viwanja vya Nyerere Square jijini humo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TARI yaelimisha wazalishaji wa karanga

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) imeanza kutoa elimu kwa wakulima wadogo wanaozalisha karanga kwenye Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Mtafiti wa zao la ufuta na karanga kutoka Kituo cha TARI, Naliendele mkoani Mtwara, Joseph Nzunda aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mafunzo ya wakulima hao.

Nzunda alisema wanatoa mafunzo hayo ili kuhakikisha wakulima wadogo wanazalisha mbegu bora ambazo zinakuwa na tija kwa wakulima.

Alifafanua kuwa takwimu za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), mwaka 2018 zinaonyesha kuwa Tanzania ilikuwa ikizalisha karanga tani 940,000 na kuwa miongoni mwa nchi 10 duniani zenye uzalishaji mkubwa wa karanga.

"Tunafundisha namna gani ya kuzalisha mbegu bora ambazo watazitoa kwa wakulima wengine kuhakikisha kunakuwa na ongezeko la uzalishaji karanga," alisema.

Alieleza kuwa uzalishaji mkubwa wa karanga utapunguza idadi ya mafuta ya kupikia ambapo asilimia 60 yanatoka nje ya nchi.

Alisema katika kituo cha TARI Naliendele wameweka mashine ya kukamua mafuta ya karanga na mashine hizo pia zinafungwa maeneo mbalimbali ili kuongeza uzalishaji wa mafuta. "Mbegu bora za karanga zinasisitizwa kuzalishwa kwa wingi kwa kuwa karanga zinahimili magonjwa mbalimbali ikiwamo ugonjwa wa ukoma kwa karanga," alisema.

Mtafiti huyo alisema ugonjwa huo huenezwa na wadudu waitwao vidukari ambapo mmea ulioshambuliwa huduma, majani hukunjamana na kuwa rangi ya manjano pia hupunguza mavuno kwa asilimia 100.

"Kudhibiti yote hayo ni kutumia mbegu bora zenye ukinzani, kupanda mapema kwa nafasi zilizopendekezwa, kukausha mavuno na kuhifadhi mahali palipo na unyevu," alisema.

Naye, mtafiti mwingine kutoka TARI Naliendele, Athanas Minja, alisema karanga ni muhimu kwa ajili ya chakula pia ni zao la biashara.

Alisema karanga ina asilimia 51.5 ya mafuta na ina kiwango kikubwa cha protini, madini ya chuma na zinki.

"Tuna aina 17 za mbegu za karanga na aina nyingine tatu maombi yapo Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na hivyo tutakuwa na mbegu aina 20," alisema. Mkulima wa zao hilo, Maria Ananias alisema wamejifunza namna bora ya kilimo cha karanga na jinsi ya kudhibiti magonjwa.

## Waliopata mikopo waonyeshwa miradi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amevitaka vikundi vilivyopata mikopo ya asilimia 10 kutoka kwenye halmashauri kuanzisha miradi yenye tija ili kujikwamua kiuchumi.

Dk. Mahenge alitoa rai hiyo alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye maonesho ya vikundi vya wajasiriamali yaliyofanyika viwanja vya Nyerere Square jijini hapa.

Aliwataka kutumia fedha hizo kuanzisha na kubuni miradi yenye tija ili kuepuka kupata hasara.

"Mnatakiwa kwanza kubuni miradi kabla ya kufikiria kuchukua mikopo vinginevyo mtachukua mikopo hiyo na kuishia kupata lawama kutokana na kushindwa kurejesha," alisema.

Alisema wananchi hao waliopata mikopo hiyo wanatakiwa kuiona kuwa ni fursa ya kuondokana na umaskini katika jamii kwa sababu inatolewa kwa na serikali.

Alibanisha kuwa vikundi hivyo vilivyokopeshwa mikopo hiyo vinatakiwa kurudisha kwa wakati ili vikundi vingine vikopeshwe.

Aidha, aliwataka wananchi hao waliopata mikopo kutumia fursa ya Makao Makuu yaliyohamia Dodoma kupanua wigo wa utoaji huduma kutokana na ongezeko la wateja.

Alisema vikundi hivyo vinatakiwa kufungua matawi maeneo mbalimbali jijini hapa ili kuwafikia wateja waliosambaa mitaa mingine na kuachana na tabia ya kujifungia eneo moja la Mji.

Naye, Meneja wa Benki ya NMB, Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema benki hiyo itaendelea kuwaunga mkono wajasiriamali kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu pamoja na kuwadhamini.

Mlozi alisema benki hiyo wametoa majaketi maalumu yatayotumiwa na madereva wa bodaboda na bajaji vijana waliopata mikopo ya pikipiki kutoka Halmashauri ya Jiji ili kutambulika wakati wakiwa kazini.

Kadhalika alisema NMB walikuwa na jukumu la kutoa elimu ya fedha kwa makundi mbalimbali yaliyopata mikopo na yanayotarajia kupata mikopo hiyo kutoka Halmashauri ya Jiji.

Kwa upande wake, Mkurungenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema zaidi ya Sh. bilioni 5.29 zimetolewa na uongozi wa Jiji hilo kwa vikundi vya watu walemavu, kinamama na vijana kuanzia mwaka wa fedha wa 2015 hadi 2020.

Mafuru alisema kati ya fedha hizo zilizokopeshwa, kiasi cha Sh. bilioni 2.5 zimesharejeshwa na zilizobaki ufuatiliaji wake unaendelea na katika hizo nyingi zilizokopeshwa katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 na vikundi vyake vipo kwenye kipindi cha marejesho.

Mkurugenzi huyo alisema katika mwaka wa fedha wa 2020/21 halmashauri hiyo imetenga kiasi cha fedha Sh. bilioni 2.23 kwa ajili ya mikopo kwa makundi hayo.

# TANGAZO

## International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA |
|---|---|---|---|
| | | 30.09.2020 | 30.06.2020 |
| A. | *MALI* | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,048 | 2,691 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 3,725 | 7,346 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 11,523 | 14,096 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,447 | 7,787 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 711 | 1,174 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 41,362 | 43,503 |
| 12 | Mali Nyingine | 5,975 | 5,360 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 470 | 503 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **67,259** | **82,460** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3,790 | 2,934 |
| 18 | Amana za Wateja | 37,670 | 56,951 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 207 | 207 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 21 | 5 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,098 | 1,277 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 61.48 | 61.22 |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,089 | 2,021 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | ***JUMLA YA DHIMA*** | **44,935** | **63,455** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **22,324** | **19,005** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 24,752 | 20,025 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 5,960 | 4,408 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5,930) | (4,377) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (2,458) | (1,051) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **22,324** | **19,005** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 2,085 | 2,357 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 16,934 | 12,187 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,747 | 1,888 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 33% | 23% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 36% | 23% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 129% | 89% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 80% | 65% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82% | 79% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -31% | 17% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -18% | 14% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 30.09.2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA LINGANISHI ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.09.2020 | 30.09.2019 | 30.09.2020 | 30.09.2019 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,073 | 1,893 | 4,287 | 5,451 |
| 2 | Gharama za Riba | 547 | 803 | 2,048 | 2,457 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***526*** | ***1,091*** | ***2,239*** | ***2,995*** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 859 | 17 | 1,520 | 77 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **282** | **203** | **928** | **705** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 14 | 40 | 96 | 33 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 45 | 47 | 143 | 144 |
| | 6.3 Gawio | | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 223 | 116 | 689 | 528 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,357** | **1,463** | **4,106** | **4,517** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 563 | 538 | 1,744 | 1,725 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 16 | 124 | 82 | 257 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 778 | 801 | 2,280 | 2,536 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,408)** | **(186)** | **(2,458)** | **(894)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | 30 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,408)** | **(186)** | **(2,458)** | **(924)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,408)** | **(186)** | **(2,458)** | **(924)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 59 | 65 | 59 | 65 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (70) | (9) | (123) | (46) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (70) | (9) | (123) | (46) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -7.54% | -0.19% | -6.59% | -0.89% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -27.32% | -0.92% | -15.58% | -4.57% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 100.16% | 69.76% | 78.73% | 73.38% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 3.50% | 4.90% | 5.02% | 5.72% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA ULIOISHIA 30.09.2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.09.2020 | 30.06.2020 | 30.09.2020 | 30.09.2019 |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,408) | (1,071) | (2,479) | (924) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 924 | 694 | 1,618 | 348 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,283 | 3,240 | 4,523 | 1,215 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (18,425) | 8,522 | (9,903) | (22,747) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (95) | 2,114 | 2,020 | 22 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (615) | (2,925) | (3,541) | 511 |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | -SMR | 1,289 | (86) | 1,203 | 808 |
| | - Mengineyo | - | 431 | 431 | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***(17,047)*** | ***10,920*** | ***(6,127)*** | ***(20,767)*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (32) | (29) | (61) | (129) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | 2,387 | (12,516) | (10,129) | (10,681) |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **2,355** | **(12,546)** | **(10,190)** | **(10,810)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 4,727 | - | 4,727 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **4,727** | **-** | **4,727** | **-** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(9,965)** | **(1,626)** | **(11,591)** | **(31,577)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 15,051 | 16,677 | 16,677 | 44,175 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **5,086** | **15,051** | **5,086** | **12,598** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

Saini:

**VILLY VELLAYAPPAN**
Ofisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: 23 Oktoba 2020

**GEORGE MSAMBAZI**
Mkuu wa Fedha
Tarehe: 23 Oktoba 2020

**JOHN MWAKASONDA**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani
Tarehe: 23 Oktoba 2020

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

Saini:

**ALFRED MKOMBO**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 23 Oktoba 2020

**CHARLES RWECHUNGURA**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 23 Oktoba 2020

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2020

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | 20,025 | - | (4,086) | 4,140 | - | - | 20,079 |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (23) | - | | | (23) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (2,458) | | | | (2,458) |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (1,821) | 1,821 | | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Mtaji wa Hisa uliotolewa | 4,727 | | | | | | 4,727 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 30.09.2020** | **24,752** | - | **(5,930)** | **5,960** | - | - | **22,324** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **20,025** | - | **(1,947)** | **2,534** | **464** | **9** | **21,085** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (924) | | | | (924) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | | | | | |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | 142 | 287 | (464) | (9) | (44) |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa kipindi 30.09.2019** | **20,025** | - | **(2,729)** | **2,821** | - | - | **20,117** |





# Polisi yaonya wasiohusika kupiga kura ya mapema leo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI leo 27 ni upigaji wa kura ya mapema, ambayo hupigwa na watu maalum kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Zanzibar, Jeshi la Polisi limewaonya wale wasiohusika kupiga kura hiyo kutokwenda vituoni.

Kamishna wa Jeshi hilo Zanzibar, Mohammed Haji Hassan, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa vyombo vya ulinzi na usalama havitarajii kumwona mtu yeyote ambaye sheria haijamtaja kupiga kura ya mapema.

Alisema kujitokeza katika vituo vya kupigia kura leo ni uvunjifu wa sheria, na hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atakayejitokeza katika vituo hivyo.

Alieleza kuwa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama linawasisitiza wananchi wakimaliza kupiga kura kesho kurudi majumbani kuendelea na shughuli zao.

"Hakuna mwananchi atakayeruhusiwa kubaki katika kituo cha kupigia kura kwa kisingizio cha kulinda kura au kwa sababu nyingineyo," alisema.

Aidha, kamishna huyo aliwataka viongozi wa vyama vya siasa na wananchi kutumia vizuri mitandao ya kijamii na kuepuka kusambaza taarifa ambazo sio za kweli zinazohusiana na uchaguzi kama kutangaza matokeo, kujitangazia ushindi au kusambaza taarifa za uchochezi.

Alisema kufanya hivyo ni kosa, na sheria itachukuliwa kwa sababu kazi ya kutangaza matokeo ni ya Tume ya Uchaguzi pekee.

Aliwatoa hofu wananchi na kusema kuwa uchaguzi utakuwa wa amani na utulivu na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vipo macho muda wote kuhakikisha amani inakuwapo kabla na baada ya uchaguzi.

"Wananchi wenye sifa ya kupiga kura mjitokeze kwa wingi Oktoba 28 mkapige kura wala msiwe na wasiwasi, ulinzi umeimarishwa kila kona," alisema.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, baadhi ya wagombea wa vyama vya siasa wamekuwa wakitoa maneno ya uchochezi, hivyo Jeshi la Polisi linachukulia matamshi hayo ni maandalizi ya uvunjifu wa amani, kwa vile yanakiuka kanuni na miongozo ya uchaguzi.

## ZEC yawaapisha mawakala wa vyama vya siasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imewaapisha mawakala wa vyama vya siasa Unguja na Pemba ambao watashiriki katika upigaji kura leo na kesho.

Kazi ya kuapisha mawakala hao kwa Wilaya ya Mjini ilifanyika katika ukumbi wa Shule ya Haile Salasie na iliongozwa na mwanasheria wa tume hiyo, Khamis Issa Khamis.

Akielezea lengo la kuapisha mawakala hao, Msimamizi wa Uchaguzi Wilaya ya Mjini, Safia Iddi Muhammad, alisema ni kuwapa fursa ya kuviwakilisha vyama vyao katika vituo vya kupigia kura.

Alisema endapo wakala yeyote hatakuwa ameapishwa kwa mujibu wa sheria na bila kuwa na kitambulisho cha uthibitisho, tume haitomtambua.

Akizungumzia kuhusu mafunzo ya watendaji wa vituo vya kupigia kura, alisema watendaji hao hivi sasa wapo tayari kufanya kazi kiufanisi baada ya kupatiwa mafunzo ya kinadharia na vitendo

Kwa upande wao mawakala waliopishwa wameahidi kufanya kazi hiyo kwa kufuata miongozo ya tume na kutoa ushirikiano wa hali ya juu baina yao na watendaji wa tume katika vituo.


**International Commercial Bank (Tanzania) Limited.**

**DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014**
**MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES As at 30th September 2020**

| PRODUCT TYPE | TZS | USD | GBP | EUR |
|---|---|---|---|---|
| **SERVICES** | | | | |
| Monthly Statement Current Accounts | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement Savings Accounts | Free | Free | Free | Free |
| E-statement | Free | Free | Free | Free |
| Interim statement - per page | 1,000 | 1 | 1 | 1 |
| **MINIMUM ACCOUNT OPENING** | | | | |
| Savings Account-Salaried | Free | Free | Free | Free |
| Savings Account-Normal | 20,000 | 50 | 50 | 50 |
| Current account-Normal | 50,000 | 100 | 100 | 100 |
| Current account -Premium | 1,000,000 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| **CASH WITHDRAWALS OVER THE COUNTER** | | | | |
| Savings account - A | | | | |
| I. Above 500,000 | Free | NA | NA | NA |
| II. Less than 500,000 | 1,000 | NA | NA | NA |
| Savings account - B | | | | |
| I. Up to USD/GBP 10,000 | NA | 5 | 5 | 5 |
| II. Above USD/GBP 10,000 | NA | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| | | | | |
| Current account | | | | |
| I. Up to 5,000,000 | Free | NA | NA | NA |
| II. Above 5,000,000 | 2,000 | NA | NA | NA |
| Current account | | | | |
| I. Up to USD/GBP 10,000 | NA | 5 | 5 | 5 |
| II. Above USD/GBP 10,000 | NA | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| Third Part withdraw per leaf | 30,000 | 30 | 30 | 30 |
| **CASH HANDLING FEE** | | | | |
| Deposits on Small Denominations Less than $50 | 3% | 3% | 3% | 3% |
| | | | | |
| **ATM WITHDRAWALS** | | | | |
| On Us | 600 | NA | NA | NA |
| On Others | NA | NA | NA | NA |
| **OTHER ATM TRANSACTIONS** | | | | |
| Issue of ATM Card(New) | 6,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card (faulty) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card (worn out) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card(Lost) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| **TRANSFERS** | | | | |
| Internal transfers | Free | Free | Free | Free |
| Interbranch Transfer | Free | Free | Free | Free |
| **STANDING ORDERS** | | | | |
| Standing orders (within bank) | 1,500 | 0.50 | 0.50 | 0.50 |
| Standing orders (to other banks Local Currency ) | 11,800 | NA | NA | NA |
| Standing orders (to other banks ) below usd 10,000 | NA | 3 | 3 | 3 |
| Standing orders (to other banks ) above usd 10,000 | NA | 10 | 10 | 10 |
| Unpaid standing orders | 40,000 | 20 | 20 | 20 |
| **CHEQUES** | | | | |
| Cheque book issuance | | | | |
| I. Personal chq book with 25 leaves | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| II.Corporate chq book with 50 leaves | 50,000 | 20 | 20 | 20 |
| III.Corporate chq book with 100 leaves | 70,000 | 35 | 35 | 35 |
| Counter cheque charges per leaf | 20,000 | 20 | 20 | 20 |
| Stop Payment orders -per instructions/ Cheque series | 40,000 | 20 | N/A | N/A |
| **Outward Cheque Unpaid (Chq returned by Us)** | | | | |
| I. Refer to Drawer | 50,000 | 50 | N/A | N/A |
| II. Effect not Cleared | 30,000 | 30 | N/A | N/A |
| III. Any Technical reason (Like endorsement) | 10,000 | 5 | N/A | N/A |
| **Inward Cheque Unpaid (Chq returned by other bank)** | 10,000 | 5 | N/A | N/A |
| Inward Cheques processing per leaf | 500 | 1 | N/A | N/A |
| | | | | |
| Bankers Cheque (account holders) | 15,000 | 10 | N/A | N/A |
| Re- Purchase of Bankers cheque on customers request | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Uncollected Cheque book (after one Month) | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| **OTHER SERVICES** | | | | |
| Current Account Closure on customer's request | 30,000 | 15 | 15 | 15 |
| Savings Account Closure on customer's request | 20,000 | 5 | 5 | 5 |
| Cheque Force clearance (with one day float) | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Chq Force clearance (with more than one day float) | 40,000 | 20 | 20 | 20 |
| Dormant Charges for Savings account | Free | Free | Free | free |
| Dormant Charges for current account | 25,000 | 15 | 15 | 15 |
| Dormant account Activations | Free | Free | Free | free |
| Account Maintanance Charge - Savings | 1,000 | 2.50 | 2.50 | 2.50 |
| Account Maintanance Charge - Current | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| Certificate of balance | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Letter of introduction | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Salary handling | Free | Free | Free | free |
| School fees deposits | Free | Free | Free | Free |
| Un arranged Temporary Overdrafts (TODs) | 24% | 10% | 10% | 10% |
| Corporate Premier Account Maintanance Charge | 20,000 | 20 | N/A | N/A |
| Individual Premier Account Maintanance Charge | 20,000 | 20 | N/A | N/A |
| Lost Cheque charges | 20,000 | 18 | 18 | 18 |
| EFT charges: | | | | |
| On Us | 300 | Free | N/A | N/A |
| On Others | 11,800 | NA | N/A | N/A |
| **TRADE FINANCE** | | | | |
| **Remittance** | | | | |
| Demand draft | NA | NA | NA | NA |
| Outward Local transfers ( TISS) | 11,800 | 11.80 | NA | NA |
| Outward Foregin transfers -Up to USD50,000 | NA | 50 | 50 | 50 |
| Outward Foregin transfers - above USD50,000 | NA | 75 | 75 | 75 |
| Inward Local transfer (TISS) | Free | Free | Free | Free |
| Inward Foreign transfer | NA | 15 | 15 | 15 |
| **Bonds & Guarantees** | | | | |
| Issuance of Bid Bond - Cash cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Issuance of Bid Bond - Other Security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Cash Cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Other security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Extentions | 1.42% Per Quarter | | | |
| Amendments | Simple amendments$50 | | | |
| Cancellations of Returned guarantees | Free | | | |
| Cancellations of guarantees if not Returned | 20,000 | | | |
| **Advance Payment Guarantees** | | | | |
| Issuance - Cash cover | 0.5% Min 100,000 | | | |
| Issuance - Security | 1.42% Min100,000 | | | |
| **Import Collections (IC)-Inward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance swift charges | Usd 50 | | | |
| **Export Collections (EC)-Outward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance Commission-per tracer | Usd 50 | | | |
| Courier Charges | Usd 100 | | | |
| **LOAN & ADVANCES** | | | | |
| Loan Processing Fees | 1.82% | | | |
| Early Loan Repayment Charges | 1% | | | |
| | | | | |
| **BASIC LENDING RATE** | 24% | 10% | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**Name:**

| | | |
|---|---|---|
| Villy Vellayappan | Chief Executive Officer | 23.10.2020 |
| Christome Tembo | Head of Operation | 23.10.2020 |
| John Mwakasonda | Head of Internal Audit | 23.10.2020 |

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**SHAMBA L INAUZWA LIPO KIBAHA KONGOWE** Shamba linauzwa lenye ekari 10 Tsh 25,000,000 lipo kibaha kongowe umbali kutoka barabarani hadi shamba KM 9 Kwa mawasiliano zaidi 0754826580.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Tunautangazia umma kuwa, kwa amri ya Mahakama Kuu ya Tanzania-Dodoma nitauza kwa mnada wa hadhara kiwanja chenye vipimo (coordinates) 1-LVR 841,LVR 842, LVR 84362-LVR 843, LVR 604, LVR 603, LVR93-LVR9, LVR 602, LVR 5,4-LVR 5, LVR 141, LVR 859 kilichopo mtaa wa MIYUJI PROPER kata ya MIYUJI JIJI LA DODOMA mali ya IBRAHIM JUMA KASIKA anayedaiwa na RASHID SEIF ABEID KILAMA ikiwa ni utekelezaji nambari 7 wa mwaka 2020. Mnada utafanyika katika eneo hilo na litauzwa kama lilivyo.

Mnada utafanyika siku ya Jumatano ya tarehe 11 Novemba 2020 saa tatu na nusu asubuhi.

Na kwa amri ya Mahakama ya Mwanzo ya Chamwino Mjini nitauza nyumba yenye kiwanja namba 753 kitalu A Ndachi Extension Manispaa ya Dodoma ukubwa wa mita za mraba 452. Nyumba itauzwa kama ilivyo.

Mnada utafanyika tarehe 14 Novemba 2020 saa nne asubuhi.

Dalali wa Mahakama ndiye mwendesha mnada, hivyo ndiye mwenye kupiga nyundo ya mwisho. Mteja mwenye bei ya juu ndiye atakayetangazwa mshindi.

Kwa mawasiliano piga 0735170553 na 0715170553 (Dalali wa Mahakama).

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
Katika Mahakama ya Mwanzo ya
NYALIKUNGU
Wilaya ya MASWA
SHAURI LA MADAI/TALAKA 38 LA 2020
MDAI: SAYI ZENGA PAULO
DHIDI YA
MDAIWA: MASANGU S/O NSESO
Kwa: MASANGU S/O NSESO WA IYOGELO – MASWA
K.K: M/KITONGOJI MWAMBAGAYA – IYOGELO
KK: MTENDAJI WA KATA BINZA - MASWA

KWA KUWA imelazimika uhudhurie ili kujibu dai la TALAKA wewe ukiwa ni mdaiwa katika shauri hili.

UNAAMRISHWA NA JAMHURI uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 03/10/2020 saa 2:30 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri liweze kusikilizwa. Usikose kuhudhuria.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 22/10/2020.

Kuitwa shaurini hii imetolewa kwa maombi ya MDAI – SAYI D/O ZENGO PAULO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DANIEL ERASTO MUNGURE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T211 CYP** Chassis namba **SXU100001090** Engine namba **5S0703029.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi
MBE/MBE/RB/757326/2020

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Vardy, Leicester waweka rekodi kuichapa Arsenal




**LONDON,** England

STRAIKA wa Leicester City, Jamie Vardy ameweka rekodi ya kufikisha mabao 22, aliyozifunga klabu sita za juu za Ligi Kuu ya England katika kipindi cha miaka mitatu akicheza jumla ya mechi 35.

Vardy alifunga bao pekee katika dakika ya 80 dhidi ya Arsenal katika mchezo wa Ligi Kuu ya England na kuiwezesha timu yake kuondoka na ushindi wa bao 1-0, Jumapili usiku.

Mshambuliaji huyo ambaye amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu msimu uliopita, pia aliweka rekodi yakuwa mchezaji wa pili kuifunga mabao mengi zaidi Arsenal ndani ya Ligi Kuu akifunga mara 11, katika michezo 12 aliyocheza dhidi ya 'Washikabunduki' hao.

Wayne Rooney ndiye mchezaji ambaye anaongoza kwa kuifunga Arsenal mara nyingi zaidi akiwa amefunga mabao 12 peke yake.

Leicester pia iliweka rekodi ya kushinda kwa mara ya kwanza nyumbani kwa Arsenal tangu mwaka 1973.

Kabla ya hapo Leicester haikuwahi kushinda kwenye mchezo wowote wa kimashindano ikiwa ugenini dhidi ya Arsenal ikiwa imecheza mechi 27.

# Umtiti agomea Barca kuondoka




**BARCELONA,** Hispania

SAMUEL Umtiti amebainisha kwamba alifanya mazungumzo na Lyon wakati wa dirisha la usajili, lakini hakutaka kuondoka Barcelona kwa ubaya.

Baada ya kuwa na mwanzo mzuri wa msimu alipotua hapo mwaka 2016 akitokea Lyon – ambako alitumia miaka 14, Umtiti amekuwa na wakati mgumu wa kuwa fiti, tangu mwanzoni mwa msimu wa 2018-19.

Amecheza mechi 77 kwenye LaLiga kwa miamba hao wa Catalunya na sasa hana namba kwenye kikosi cha kwanza.

Kurudi Lyon ndio jambo lililokuwa linaonekana msimu uliopita, lakini Umtiti hakutaka kwanza kuondoka hapo Camp Nou.

"Kila kitu kilikuwa kinawezekana kwa ajili ya uhamisho wa dirisha lililopita," alisema akiiambia Canal+. "Lyon ni klabu yangu na jiji langu. Walinipa nafasi ya kuanza na kuonekana pale.

"Kulikuwa na majadiliano, lakini ilikuwa haraka, hakuna kilichokamilika. Nilitakiwa kwanza kuzungumza na klabu. Kwa ukweli: Barcelona ni Barcelona.

"Sitaki kuondoka Barcelona kwa namna yoyote mbaya kwa sasa."

Umtiti hadi sasa hajaanza mchezo wowote msimu huu chini ya kocha mpya wa Barca, Ronald Koeman.

Hata hivyo, nyota huyo mwenye umri wa miaka 26, ana matumaini kuwa majeruhi kwa namna moja yamebadilisha maisha yake ya uchezaji na ana imani atapata tu nafasi

# De Beek hakupaswa kutua UTD - Van Basten




**AMSTERDAM,** Uholanzi

DONNY van de Beek hakutakiwa kujiunga na Manchester United wakati huu, huku sasa akipambana kupata nafasi ya kucheza pale Old Trafford, amesisitiza gwiji wa Uholanzi, Marco van Basten.

Van de Beek bado hajaanza mchezo wowote wa Ligi Kuu ya England kwa United baada ya kuwasili kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, Ajax mwanzoni mwa msimu huu kwa dili lililogharimu kiasi cha pauni milioni 39.1.

Hakutumiwa kwenye mchezo wa Jumamosi wa sare dhidi ya Chelsea, wakati Van de Beek akiwa amecheza kwa dakika 60 katika mechi nne za Ligi Kuu, na mashaka zaidi sasa yakiibuliwa juu yake pale Manchester.

Van de Beek, ambaye awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na Real Madrid, alicheza dakika mbili za mwisho kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain, huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, akiwa ameanza kwenye mechi zote za Kombe la EFL.

Gwiji wa zamani wa Ajax, AC Milan na Uholanzi, Van Basten akizungumzia kuhusu hali ya Van de Beek pale Man United alisema: "Donny hakutakiwa kwenda Manchester United."

"Wakati ukiwa mchezaji mzuri unataka kucheza kila wiki. Kwa hakika ni kitu kibaya kwa mchezaji kama Donny kucheza mechi sita au saba tu kwa mwaka huu. Hiyo inaondoa ubora wake."

# Pirlo haihofii Barcelona UEFA



**TURIN**, Italia

ANDREA Pirlo amesisitiza hana hofu kuhusu Barcelona baada ya Juventus kutoka sare nyingine kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Juve ilihitaji bao la dakika ya 77 kutoka kwa Dejan Kulusevski ili kusawazisha na kupata sare ya 1-1 nyumbani dhidi ya Hellas Verona, ambao walitangulia kwa bao la Andrea Favilli, Jumapili.

Mabingwa hao wa Serie A hawajashinda katika mechi mbili mfululizo za ligi na mara ya kwanza dhidi ya Verona tangu mwaka 1989 na Juve walifikisha pointi tisa baada ya mechi tano.

Juve watawakaribisha Barca kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Jumatano, lakini Pirlo hana hofu nao, akisema anatarajia mchezo tofauti kabisa.

"Hapana, siwahofii Barcelona, kwa sababu ni timu zinazokutana zikiwa na mchezo tofauti kabisa na hiyo ni ligi tofauti pia," alisema Pirlo akiwaambia waandishi wa habari.

"Kama nilivyosema mapema, Atalanta kama Verona wanacheza soka tofauti kabisa ukilinganisha na Barcelona, kwa hivyo kama unacheza na timu kama ile unakuwa ni mchezo wa tofauti kabisa.

"Unatakiwa kujaribu vitu fulani, kitu ambacho tulijaribu kukifanya kwenye mchezo ule."

Matokeo hayo yameifanya Juve kupitwa pointi tatu na vinara AC Milan, ambao jana Jumatatu walikuwa wakicheza dhidi ya AS Roma.

## Lizarazu: Griezmann ondoka Barcelona

**PARIS,** Ufaransa

ANTOINE Griezmann ameshauriwa kuondoka Barcelona na mlinzi wa kushoto wa zamani wa Ufaransa, Bixente Lizarazu.




Baada ya kujiunga na Barca kutoka Atletico Madrid kwa euro milioni 120 Julai mwaka 2019, Griezmann amefunga mabao 15 katika mechi 48 kwenye mashindano yote msimu uliopita, ukiwa ni mwanzo mbaya tangu msimu wa 2012-13 akiwa na Real Sociedad.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 29, ana wastani wa kufunga bao moja kwenye La-Liga kila dakika 285 kwa Blaugrana hao, kutoka wastani wa dakika 112 wakati akiwa kule Atletico mwaka 2014-15.

Kwa sasa amekuwa akichezeshwa kama winga ya kulia chini ya kocha Ronald Koeman na alicheza dakika nane tu wakati wa mchezo wa Clasico huku Barca ikichapwa mabao 3-1 na Real Madrid, Jumamosi.

Na sasa mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, Lizarazu anaamini Griezmann, ambaye ameripotiwa kujiandaa kusaini mkataba mpya pale Camp Nou, anatakiwa kuondoka kabla mambo hayajawa mabaya zaidi.


"Griezmann ni mchezaji mkubwa. Ni mchezaji mzuri na amefanya makubwa kwa Ufaransa.

"Lakini yule anayecheza pale Barcelona si yeye. Na hilo ni tatizo kubwa kwake," alisema Lizarazu akiiambia Telefoot, Jumapili.

"Alikwenda Barcelona akiwa na ndoto ya kucheza pamoja na Lionel Messi, lakini bahati mbaya hakuna uhusiano mzuri wa kiufundi kati ya wawili hao.

"Hawezi kupata nafasi, hawezi kuendelea kucheza soka na Barca. Kuna tatizo la kujiamini. Ni wakati muafaka kwake sasa kuondoka Barcelona na kutafuta changamoto nyingine."

# Fabinho amshukuru Klopp kumbadilisha




**LIVERPOOL,** England

FABINHO amefichua kwamba, kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp amembadilisha kuvaa viatu vya Virgil van Dijk, baada ya beki huyo wa kati kuumia goti.

Fabinho mwenye umri wa miaka 26, alikuwa na mchezo mzuri dhidi ya Ajax katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano iliyopita, akirudishwa katika nafasi ya ulinzi wa kati kwa kucheza pamoja na Joe Gomez.

Pamoja na kufanya ukabaji mzuri na umakini, Fabinho aliokoa vizuri mchomo wa Dusan Tadic katika kipindi cha kwanza.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil, ambaye kwa kawaida hucheza kama kiungo, sasa amesema Klopp alimwambia kuwa mzungumzaji, hasa akiwa anacheza kama beki wa kati.

"Kiufundi, nilitakiwa kuwa tayari kwa mipira mirefu na kujaribu kuunganisha timu," alisema alipohojiwa na Viaplay.

"Haikuwa rahisi, lakini nilitakiwa kufanya kidogo kati ya vile ambavyo Virgil anavyofanya kila siku, kuzungumza na timu na kuwaweka pamoja.

"Ni kweli kwamba siwezi kuiga kila kitu, lakini nitajitahidi. Ilikuwa muhimu kwangu na timu kwa ajili ya kutoruhusu bao, na hiyo imenipa kujiamini."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YALILIA BAO LA LACAZETTE LEICESTER

## Arteta asema hajui kwa nini lilikataliwa, asifu walishinda kila mpira na kutengeneza nafasi, lakini...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amehoji maamuzi ya kukataliwa bao lao la mapema kupitia kwa Alexandre Lacazette wakati Arsenal ikifungwa 1-0 na Leicester City kwenye dimba la Emirates, Jumapili usiku.

Lacazette alifunga kwa kichwa katika dakika ya nne ya mchezo huo wa Ligi Kuu ya England, lakini lilikataliwa kwa sababu wachezaji wenzake wa Arsenal, Granit Xhaka na Pierre-Emerick Aubameyang walionekana kuwa wameotea.

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa, Lacazette baadaye alikosa nafasi kubwa katika kipindi cha kwanza na Arsenal wakajikuta kwenye wakati mgumu wakati Leicester walipomwingiza Jamie Vardy aliyefunga bao pekee kwenye mchezo huo zikiwa zimebaki dakika 10 mpira kumalizika.

Lakini wakati Arteta hakuwa na furaha na maamuzi ya kukataliwa kwa bao la Lacazette, kocha huyo wa 'Washikabunduki' alikubali kwamba, mengi zaidi yanatakiwa kufanywa kwenye kikosi hicho kutokana na Arsenal kufungwa michezo mitatu mfululizo kwenye ligi hiyo.

**"Mchezo ulikwenda namna ulivyokuwa. Nahisi tulitawala zaidi kipindi cha kwanza, lakini hatukufanya lolote kuweza kupata ushindi," alisema Arteta akiiambia BBC Sport.**

"Tulikuwa tunashinda kila mpira, tulitengeneza nafasi chache za kufunga na tukafunga bao - sijui kwa nini lilikataliwa.

"Walizuia vizuri kipindi cha pili, wakisubiri nafasi moja tu ya sisi kufanya kosa na ndivyo ilivyotokea."

Akielezea kuhusu bao hilo kukataliwa wakati akizungumza na waandishi wa habari, Arteta aliongeza: "Granit kuwa nyuma ya (Kasper) Schmeichel halikuwa tatizo lolote.

"Walifanya maamuzi na hatuwezi kuyabadilisha kwa sasa."

Leicester ilishindwa kutengeneza nafasi ya kufunga kabla ya kuingia kwa Vardy, na haraka alipoingia alitumia vizuri krosi ya Cengiz Under na kufunga bao lake la 11 la ligi dhidi ya Arsenal.

## KWA UFUPI

### DYAALA KUJIFUNGA JUVENTUS
NYOTA wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 26, ambaye amehusishwa na uhamisho wa kuelekea Tottenham pamoja na Manchester United, yuko katika mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Italia. (Sky Sports)

### MODRIC AKATAA KURUDI SPURS
KIUNGO wa kati wa Real Madrid na Croatia, Luka Modric mwenye umri wa miaka 35, amesisitiza kwamba yeye ni mzee sana kufuata nyayo za mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale kwa kurudi Tottenham. (FourFourTwo via Marca)

### MBAPPE SI WAKUONDOKA PSG
STRAIKA wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21, ana mipango ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na klabu ya PSG kabla ya kuhamia katika klabu nyingine kubwa, kwa mujibu wa kiungo wa zamani wa PSG ambaye kwa sasa ni balozi wa klabu hiyo, Youri Djorkaeff. (Goal)

### ARTETA AMFUNGUKIA OZIL
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema amekuwa wazi kwa kiungo wa kati wa Ujerumani, Mesut Ozil, mwenye umri wa miaka 32, licha ya wakala wa mchezaji huyo kudai kwamba, kumekuwa hakuna uwazi kuhusu mchezaji huyo kuachwa nje ya kikosi cha timu hiyo. (Mirror)

### UPAMECANO ATAJWA UNITED
KLABU ya Manchester United ilikosa kumsajili beki wa RB Leipzig na Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, Dayot Upamecano - ambaye kwa sasa ana thamani ya pauni milioni 55, kwa sababu ya mgogoro wa kuhusu pauni 200,000 miaka mitano iliopita. (Sun)

### LIVER KUTOSAJILI BEKI JANUARI
LIVERPOOL huenda ikaamua kutomsaini beki wa kati Januari na kusubiri kupata mchezaji atakayedumu msimu ujao, licha ya kumkosa Virgil van Dijk atakayekaa nje kwa muda mrefu. (Liverpool Echo)

### MAHREZ SASA AIKANA PSG
WINGA wa Manchester City na Algeria, Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 29, amekana madai katika vyombo vya habari vya Ufaransa kwamba alizungumzia uwezekano wa kujiunga na PSG. (Manchester Evening News)

### ARSENAL MASHAKANI KWA AOUAR
ARSENAL ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Lyon na Ufaransa, Houssem Aouar, mwenye umri wa miaka 22, lakini inakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa Paris St-Germain na Juventus. (Tuttosport - in Italian)

### MILIK KUSEPA NAPOLI JANUARI
MSHAMBULIAJI wa Poland, Arkadiusz Milik, ambaye alikuwa tayari kujiunga na Juventus msimu ujao, ataondoka Napoli Januari huku klabu za Tottenham na Everton zikimnyemelea mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (Calciomercato via Mail)

### SHEFFIELD YAMWANIA ROJO
KLABU ya Sheffield United inataka kumsajili kwa mkopo beki wa Manchester United na Argentina, Marcos Rojo mwenye umri wa miaka 30, wakati wa dirisha la Januari. (Sun)

### SHELVEY AIPA PIGO NEWCASTLE
KIUNGO wa kati wa Newcastle na England, Jonjo Shelvey mwenye umri wa miaka 28, anakabiliwa na jeraha la nyonga ambalo huenda akafanyiwa upasuaji. (Newcastle Chronicle)

# KAZE AELEZA SIRI STRAIKA WAWILI KUIBEBA YANGA

**Na Adam Fungamwangoo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema amegundua kuwa viwanja vya mikoani kama timu inataka kufanya vizuri ni lazima achezeshe mastraika wawili kutokana na namna vilivyo na jinsi timu nyingi zinavyolazimika kucheza mipira mirefu.

Akizungumza baada ya mechi kati ya timu hiyo dhidi ya KMC ambayo walishinda mabao 2-1 katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Kaze raia wa Burundi ambaye hiyo ni mechi yake ya pili kuiongoza Yanga huku zote akiibuka na ushindi, alisema timu nyingi wanazocheza nazo zikicheza kwenye viwanja hivyo mara nyingi hucheza mipira mirefu, hivyo inakuwa ngumu kucheza na straika mmoja, jambo ambalo aliamua kumtumia Waziri Junior kama straika wa pili, huku Michael Sarpong akiwa namba moja na matunda yake kuonekana.

"Nimemtumia Waziri kama straika wa pili kwa sababu ya aina yake ya uchezaji, hakai sehemu moja, anarudi chini na pembeni, anacheza wakati mwingine kama kiungo na pia anafika kwenye eneo la hatari haraka, hivyo tukafanikiwa," alisema.

Pamoja na ushindi huo, kocha huyo alisema kuna tatizo ameliona, kwani baada ya kufunga bao la pili, wachezaji wake wakaacha kucheza mpira na kushambulia, badala yake wakageukia kuzuia tu, kitu ambacho alisema si kizuri na atakiangalia na kukifanyia kazi.

Kuhusu kubadilisha kikosi mara kwa mara, kocha huyo alisema kuwa si kwamba hajapata kikosi cha kwanza, bali anafanya hivyo ili kuwapumzisha baadhi ya wachezaji kutokana na mfululizo wa mechi.

"Siku 12 tunacheza mechi nne, hii si sawa, hakuna mchezaji anaweza kucheza mechi nne kwa siku 12, ndiyo maana tunawapunguzia wachezaji wetu muda wa kucheza na kuwabadilisha," alisema Kaze.

Kwenye mechi yake ya kwanza, kaze aliiongoza Yanga kushinda bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania.

Yanga inashika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ikiwa na pointi 19, baada ya kucheza mechi saba, kushinda sita na kutoka sare moja.

Wakati Kaze akigundua hilo muda mfupi tu baada ya kuwasili nchini, hivi karibuni wanachama na mashabiki wa Simba walikuwa wakimlalamikia kocha wao, Sven Vandenbroeck kwa kupenda kuchezesha straika mmoja, hasa anapokuwa kwenye viwanja vya mikoani ambavyo vingi havina ubora, na siku alipoamua kufanya hivyo kwenye mechi dhidi ya JKT Tanzania, Simba iliibuka na ushindi mkubwa ugenini wa mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma, ikiwachezesha Meddie Kagere na Chriss Mugalu ambao wote walifunga.

**SAMATTA KAZINI...**



Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akishangilia na wachezaji wenzake wa Fenerbahce kwa kuwarukia juu, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Trabzonspor kwenye mechi ya Ligi Kuu Uturuki iliyopigwa Uwanja wa Fenerbahce Sukru Saracoglu Sports Complex, jijini Istanbul usiku wa kuamkia jana. Mabao ya Fenerbahce yalifungwa na beki Serkan Asan aliyejifunga dakika ya 51, washambuliaji Enner Valencia (dk. 55) na Papiss Cisse (dk. 72) wakati lile la Trabzonspor likifungwa na Mkongomani Benik Afobe dakika ya 23. **PICHA: MTANDAO**

# Biashara yaanza kuitisha Yanga Musoma

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amesema ushindi wao dhidi ya Polisi Tanzania hautawafanya kubweteka, bali utawaongezea ari kuelekea mechi dhidi ya Yanga, utakaopigwa Jumamosi katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mkoani Mara.

Biashara juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 ikiwa ugenini katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha dhidi ya Polisi Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana akiwa njiani kuelekea Musoma Baraza alisema hawezi kuihofia Yanga kwa kuwa safu ya ushambuliaji inaundwa na wachezaji wengi wageni ambao hawaifahamu vema timu yake.

"Yanga hainipi hofu kwa sababu ni timu ya kawaida kama zilivyo timu nyingine ambazo zinashiriki Ligi Kuu," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema ameifuatilia timu hiyo michezo yake ambayo imeicheza na kutambua sehemu ambazo wanatakiwa kuwabana ili wasipate nafasi ya kuwafunga, lakini akikiri mchezo huo utakuwa mgumu kwani kila timu inahitaji ushindi ikiwa ni pamoja Yanga kuundwa na wachezaji wazuri.

Alisema ana imani na wachezaji wake kufanya vizuri na kuhakikisha mechi hiyo ijayo vijana wake watapambana kutafuta matokeo mazuri na kubakiza pointi muhimu wakiwa nyumbani.

"Tumepata pointi tatu, ugenini dhidi ya Polisi, wachezaji wamecheza vizuri na sasa tunaenda kujipanga kuhakikisha tunafanye vizuri katika mechi yetu hiyo," alisema Baraza.

## Ligi Kuu Zanzibar yapigwa kalenda

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesogeza mbele mchezo wa Ngao ya Jamii ambao ni maalum kwa ajili ya kufungua rasmi msimu mpya wa 2020-2021 wa Ligi Kuu Zanzibar, lakini pia tarehe ya kuanza kwa ligi hiyo nayo ikisogezwa mbele hadi Novemba 14, mwaka huu.

Kama inavyoonekana katika kalenda ya ZFF, mechi hiyo ambayo ilikuwa imkutanishe bingwa wa Ligi Kuu, Mlandege na bingwa wa Kombe la Shirikisho, KVZ FC, sasa itachezwa Novemba 8, mwaka huu badala ya Novemba Mosi kama ilivyokuwa imepangwa hapo awali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohmmed Ameir, imeeleza kuwa shirikisho hilo pia limesogeza mbele tarehe ya kuanza Ligi Kuu Zanzibar, ambapo sasa itaanza Novemba 14, mwaka huu badala ya Novemba 7, huku Ligi Daraja la Kwanza Kanda ikitarajiwa kuanza Novemba 21, mwaka huu.

Taarifa hiyo ilieleza sababu ya kusogezwa mbele kwa tarehe za ligi hiyo ni kupisha kumalizika kwa harakati za uchaguzi, ili waamuzi wapate nafasi ya kufanya mtihani wa utimamu wa mwili (Copa test) ambapo nao umepangwa kuanza wiki ya kwanza ya Novemba.

Aidha, ilieleza pia kuwa Uwanja wa Amaan ambao ZFF imekuwa ikiutumia kwa mechi za ligi, kwa sasa unaotumika kwa shughuli za kiserikali.

## ZFF yataja sifa za makocha Ligi Znz

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limezitaka klabu za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza visiwani hapa, kuhakikisha wanakuwa na makocha wenye sifa ambazo zimeainishwa katika kanuni za mashindano ya ZFF kwa msimu huu wa 2020-2021.

Kwa mujibu wa kanuni hizo, kocha anayefundisha klabu yoyote ya Ligi Kuu Zanzibar ni lazima awe na leseni Daraja A ama B wakati anayefundisha Ligi Daraja la Kwanza Kanda akipaswa kuwa na leseni kuanzia Daraja C kupanda juu.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohmmed Ameir, alisema bado timu zimeendelea kuwa na walimu ambao hawana sifa za kufundisha madaraja hayo na kwamba zinapaswa kutambua kuwa kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa kanuni ya mashindano.

Alisema ZFF kupitia Kamati ya Mashindano haitasita kufuata kanuni pale timu yoyote itakayokwenda kinyume cha kanuni ikiwamo kuwa na walimu ambao hawana sifa ya kufundisha madaraja hayo hususan kwa zile za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza Kanda.

Michezo
Jumanne Oktoba 27, 2020
Nipashe




Arsenal yalilia bao la Lacazette kwa Leicester

# Penalti ya Yanga kuna tatizo - Refa

Na Mwandishi Wetu

HUKU Kocha wa KMC FC, Habibu Kondo, akieleza penalti tata iliyotolewa na Mwamuzi Ramadhani Kayoko wa Dar es Salaam katika mchezo wao dhidi ya Yanga, ndiyo ilichangia kuwaondoa mchezoni wachezaji wake na kujikuta wakipoteza kwa mabao 2-1 juzi, Refa mstaafu, Omar Abdulkadir, amesema "kuna tatizo".

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi, Yanga ilishtukizwa kwa kufungwa bao dakika ya 26 kupitia kwa Hassan Kabunda kwa shuti kali nje ya 18, kabla ya Tuisila Kisinda kuisawazishia timu yake kwa mkwaju wa penalti dakika ya 41 akimtesa kipa mkongwe Juma Kaseja baada ya refa Kayoko kudai straika Mghana Michael Sarpong aliangushwa ndani ya boksi.

Dakika ya 61, Waziril Junior akaifungia Yanga bao la pili likiwa ni la kwanza kwake msimu huu tangu ajiunge na klabu hiyo akitokea Mbao FC, hivyo kuifanya KMC kutoka kichwa chini.

Lakini kocha Kondo, akizungumzia ushindi huo wa Yanga, alisema tatizo ilikuwa ni penalti hiyo ambayo kwake anaona haikuwa halali na kwamba ndiyo iliyowarudisha wapinzani wao mchezoni na hatimaye kushinda.

"Tatizo kwetu lilikuwa ni bao la pili, tumefanya makosa tukafungwa, ila la kwanza haikuwa penalti, kawapa wakafunga ikawarudisha mchezoni, lakini hamna shida ligi ni kama marathon bado mechi nyingi kwetu zimebaki 30," alisema.

Lakini refa mstaafu, Abdulkadir, ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Saa 72 ya TFF, alipotakiwa kutoa maoni yake kuhusu penalti hiyo, alisema kuna tatizo la waamuzi Tanzania, ila hawezi kuizungumzia kabla hawajakaa katika kamati hiyo.

"Nimeangalia sana, ila Tanzania kuna tatizo kubwa, hakuna waamuzi, siwezi kuizungumzia kwa sasa, kabla ya kamati kukaa, nikiongea lolote kwa sasa itakuwa si sahihi," alisema Abdulkadir huku akifafanua kuwa kamati hiyo hukutana kila wiki.

PATASHIKA...



Patashika ya wachezaji wa Simba na Ruvu Shooting wakizozana baada ya kiungo wa Wekundu wa Msimbazi, Luis Miquissone kuchezewa rafu mbaya eneo la hatari kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jana na Ruvu kushinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YAPAPASWA, AZAM IKIFIA MTIBWA

## ●●● Mechi yageuka ya kibabe Uhuru, huku Wanalambalamba nao wakilambishwa...

**Adam Fungamwango,** DAR **na Saada Akida,** MOROGORO

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakipoteza mechi yao ya pili mfululizo baada ya jana kukubali kulala kwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Mtibwa Sugar nayo imewatuliza vinara wa ligi hiyo, Azam FC kwa kichapo kama hicho katika dimba la Jamhuri mjini Morogoro.

Kipigo hicho kinaifanya Simba kuendelea kupata tabu dhidi ya timu za majeshi baada ya Alhamisi iliyopita, kupoteza mechi yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu ilipotandikwa bao 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga.

Lakini, ushindi huo kwa Ruvu Shooting ni mwendelezo wa kufanya vizuri baada ya mchezo uliopita kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC, huku wababe waliopita wa Simba, Prisons nao jana wakiendeleza ushindi kwa kuichapa Dodoma Jiji bao 1-0 kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa.

Katika mechi ya Simba na Ruvu Shooting, alikuwa ni Fully Maganga aliyepeleka msiba Msimbazi, akifunga bao dakika ya 35 baada ya timu yake kufanya shambulizi la kushtukiza.

Baada ya Simba kufanya mashambulizi mfululizo kwenye lango la Ruvu Shooting, ulipigwa mpira mrefu ambao ulisababisha kizaazaa kwenye lango la Simba na kumkuta mfungaji aliyeachia shuti la karibu lililomshinda kipa Beno Kakolanya na kajaa wavuni.

Kuanzia dakika ya 70, mechi hiyo ilisimama kwa muda kutokana na wachezaji wa pande zote mbili kusukumana kwa hasira, hali hiyo ikitokana na mchezaji wa Ruvu kumchezea rafu Luis Miquissone ambayo ilizaa penalti.

**Hata hivyo, nahodha wa timu ya Simba, John Bocco, ambaye ni aghalabu sana kukosa penalti, aligongesha mlingoti wa juu na kurejea uwanjani dakika ya 78, akiikosesha timu yake bao la kusawazisha.**

Mechi ilianza kwa kasi na dakika ya sita, Ibrahim Ajibu aliunganisha kwa kichwa mpira wa krosi kutoka kwa Larry Bwalya, lakini ulitoka kidogo nje la lango la Ruvu Shooting.

Dakika ya 20, Abdulrahman Mussa alibaki yeye na kipa Kakolanya, lakini alipiga nje. Likuwa ni shambulizi la kushtukiza baada ya Simba kufanya mashambulizi mfululizo kwenye lango la Ruvu Shooting.

Luis Miquissone, alikosa bao la wazi dakika ya 34 alipobaki yeye na kipa wa Ruvu, lakini akamlenga na kipa akaudaka kirahisi mpira huo. Dakika moja kabla ya mapumziko, Shomari Kapombe aliikosesha Simba bao la kusawazisha akiwa amebaki na lango akapiga mpira juu.

Kipindi cha pili, Simba iliwatoa Bwalya na Francis Kahata na nafasi zao kuchukuliwa na Bocco, pamoja na Bernard Morrison, licha ya kujitahidi kuleta uhai, lakini mabeki wa Ruvu Shooting wakiongozwa na Juma Nyosso walikaa imara kuokoa hatari zote, huku wakitumia nguvu zaidi kuwazuia wachezaji wa Simba.

Kwingineko katika Uwanja wa Jamhuri, Morogoro, wenyeji Mtibwa Sugar waliwaonjesha vinara wa Ligi Kuu, Azam FC kipigo cha kwanza msimu huu kwa kichapo cha bao 1-0, shukrani kwa Jafar Kibaya aliyewazamisha dakika ya 61 kwa shuti kali la mbali ambalo lilimshinda kipa David Kisu.

Kwa matokeo hayo ya jana Simba inabaki na pointi zake 13, ikiwa nafasi ya nne wakati Azam nayo ikiendelea kubaki kileleni na alama zake 21, Tanzania Prisons inapanda hadi nafasi ya tano ikiwa na pointi 12, huku Ruvu Shooting yenye pointi 12 ikiwa nafasi ya saba na Mtibwa nafasi ya 10 ikiwa na alama 11.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >